SportPesa
TZS. 642,668,240
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**MASHARTI** mafao waliofutwa kazi uhakiki wa vyeti

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Novemba 6, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580756
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia: Nadra kumpata mtu kama Maalim Seif

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia kwenye ufunguzi wa Kongamano la Kumbukizi ya Maisha ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT-Wazalendo na Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## KESI YA MBOWE

# Kibatala aibua jambo

**AHOJI** uhusiano wa Sabaya na askari aliyefukuzwa kazi kukamata washtakiwa... *Endelea ukurasa wa 2*

## Maagizo matatu ya Bunge baa la njaa

UKURASA 3

MICHEZO NABI - MOTO WA YANGA HAUZIMIKI UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akipata maelezo kutoka kwa Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Zanzibar, Rashid Mzee Abdallah (kulia), juu ya hatua walizozichukua lilipotokea tukio la moto katika Taasisi ya Sayansi za Bahari ya chuo hicho hivi karibuni, wakati alipofanya ziara ya kukagua athari za moto huo chuoni hapo, Mizingani, Wilaya ya Mjini juzi. Habari zaidi Uk. 10. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wakili Kibatala aibua jambo

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa saba wa Jamhuri katika kesi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu, Inspekta Mahita Omary, amekana kuwateka watuhumiwa, akidai waliwakamata na walipopekuliwa hawakukutwa na pochi wala fedha.

Mshtakiwa Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya katika ushahidi wao kwenye kesi ndogo, walidai askari polisi waliwapekua na kuchukua simu zao pamoja na fedha zaidi ya Sh. 300,000.

Vilevile, Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, ameibua jambo alipohoji sababu za kutoamini kuwa Inspekta Mahita, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya kwa kushirikiana na ACP Kingai na Afande Goodluck, wamembambikia Mbowe kesi kwa ajili ya mambo ya kisiasa baina ya Mbowe na Sabaya.

Inspekta Mahita alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga wakati akihojiwa na Wakili wa Utetezi, John Mallya.

Wakili huyo alitaka shahidi aeleze kuhusu madai ya washtakiwa kuwa walitekwa, hawakukamatwa na walikuwa na pochi yenye fedha mifukoni mwao.

Mahita alidai hawakuwateka bali waliwakamata na alishuhudia upekuzi lakini watuhumiwa, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya hawakuwa na vitambulisho wala fedha.

Alidai kuwa aliwahi kukamata magaidi Arusha lakini hakumbuki walionyesha gaidi gani mwenzao na katika kuwatafuta watuhumiwa, alifika hadi Tabora.

Akihojiwa na Wakili Jeremiah Mtobesya, shihidi huyo alidai taarifa kuhusu watuhumiwa alikuwa akiambiwa na Kamishna Msaidizi wa Polisi Ramadhan Kingai na Kingai alikuwa akizipata kwa msiri wake.

Alidai kwa uelewa wake, Kingai alikuwa mtu wa kwanza kupokea taarifa za watuhumiwa lakini alidai si jukumu lake kuzithibitisha kutoka kwa chanzo hicho.

Shahidi alikiri kuwa eneo la Rau Madukani, mahali walipokamatwa watuhumiwa, liko 'bize' na kuna mwingiliano wa watu wengi.

Alipohojiwa kama anafahamu kuna kielelezo mahakamani, kinadai washtakiwa Julai 24, mwaka 2020 walikuwa Moshi na Julai 31, mwaka huo walitoka Moshi kuelekea Dar es Salaam, shahidi alijibu kuwa hafahamu.

Akihojiwa na Wakili Peter Kibatala, shahidi huyo alidai katika ushahidi wake hakusema maandamano ya bila ukomo yaliyotakiwa kufanywa Mkoa wa Morogoro yalikuwa yafanyike maeneo mengine.

Shahidi alidai ACP Kingai hajawahi kumwambia kwamba msiri wake ni Luteni Urio na katika hati ya mashtaka inaeleza matukio ya ugaidi yalitakiwa kufanyika Morogoro, Arusha, Dar es Salaam na Mwanza, lakini katika ushahidi wake hakueleza kama kuna mpelelezi aliwahi kufika Mkoa wa Morogoro, Mwanza na Mbeya. Katika ushahidi wake, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, Inspekta Mahita alidai Agosti 4, mwaka 2020 alipigiwa simu na ACP Kingai akaambiwa wanaenda kufanya kazi Moshi, hivyo atafute askari wawili, akawatafuta afande Goodluck na Francis.

Alidai walimpitia Afande Jumanne Usa River kuelekea Moshi ambako walifahamishwa kuna kikundi cha watu kinataka kufanya vitendo vya kigaidi, wanapanga kumdhuru Lengai Ole Sabaya, hivyo waende wakazuie.

Inspekta Mahita alidai walianza safari saa mbili au tatu usiku, walifika Moshi lakini kwa siku hiyo hawakufanikiwa kuwapata hadi kesho yake walipofahamishwa kuwa wako Rau Madukani.

"Tulipofika Rau Madukani Agosti 5, mwaka 2020, tulijigawa makundi mawili - kundi moja Afande Kingai, Jumanne na Goodluck na kundi la pili mimi na Francis.

"Watuhumiwa walikuwa upande waliokuwa kina afande Kingai lakini naona waliwaona wakasimama wakaja upande wangu tukawasimamisha, nilitumia sauti ya ukali, walisimama na watu waliokuwa karibu walisikia. "Tuliambiwa wako watatu lakini walisimama wawili, nilijitambulisha na kuwafahamisha wanatuhumiwa kwa ugaidi, afande Jumanne naye alikuja akajitambulisha kisha aliwapekua wote wawili na kuandika hati ya upekuzi ambayo ilisainiwa na watuhumiwa pamoja na mashahidi.

"Mshtakiwa Kasekwa alikuwa na pisto, risasi tatu, simu yenye line ya Voda na Airtel na kete 58 za dawa za kulevya, Mohammed Ling'wenya alikutwa na kete 25 na simu," alidai Mahita.

Alidai walishirikiana nao kumtafuta mshtakiwa Moses Lijenje bila mafanikio, wakawarudisha Kituo cha Polisi cha Kati Moshi hadi Agosti 6 usiku walipowasafirisha kuwapeleka Dar es Salaam ambapo walifika Agosti 7, mwaka 2020.

Shahidi alidai waliwafikisha Kituo Kikuu cha Polisi kisha wakawahamishia Kituo cha Polisi Mbweni ambako kuna ulinzi tofauti kutokana na mafunzo ya ukomandoo waliyokuwa nayo washtakiwa waliona kunawafaa kwa kuwaweka kila mshtakiwa katika chumba chake.

Alidai kuwa mshtakiwa Alfani Bwire alikamatwa ndani ya gari eneo la Chang'ombe, Dar es Salaam.

Alidai Bwire alikamatwa Agosti 9, mwaka 2020 majira ya saa 2 usiku, baada ya aliyekuwa Mkuu wa Polisi Mkoa wa Arusha, ACP Kingai kupanga askari wa usalama barabarani eneo hilo waliokuwa wakikagua magari.

Alidai Bwire wakati anakamatwa, alikuwa amekaa katika siti ya katikati, alitolewa kisha kupelekwa katika Kituo cha Polisi Chang'ombe.

JAMBO LA KIBATALA

Baadaye Wakili Kibatala alihoji kwa nini wasiamini kuwa Inspekta Mahita, Sabaya kwa kushirikiana na ACP Kingai na Afande Goodluck wamembambikia Mbowe kesi kwa ajili ya mambo na kisiasa baina ya Mbowe na Sabaya.

Akijibu swali hilo, Inspekta Mahita alidai kazi ya polisi sio kusingizia watu kesi bali kufanya uchunguzi na upelelezi wa matendo ya kihalifu.

Inspekta Mahita pia alidai hafahamu kama Afande Jumanne ambaye alishirikiana naye katika kuwakamata washtakiwa Adam Kasekwa, Mohamed Ling'wenya na Halfani Bwire alifukuzwa kazi kwa tuhuma za kuongozana na genge la Sabaya.

Pia alidai hafahamu kwamba anatuhumiwa kumwekea mzee mstaafu Profesa Justine Maeda meno ya tembo kwenye eneo la nyumba yake.

Vilevile, alidai hakuwahi kumfahamisha Sabaya kuhusu suala lake la kudhuriwa na hawakuwasiliana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, taifa au kutoa taarifa kwa Idara ya Usalama wa Taifa juu ya njama hizo za ugaidi.

Akielezea ushahidi aliotoa, alidai hakumwambia jaji vikao gani vilifanyika Aishi Hotel, hakumwambia ni Morogoro sehemu gani washtakiwa walikaa kupanga njama za kufanya ugaidi.

Shahidi alidai hakumwambia jaji kama mshtakiwa Mbowe na wenzake walikaa Arusha na Dar es Salaam wakapanga njama za kufanya ugaidi.

Akiendelea kuhojiwa na Kibatala, shahidi alidai hakuwahi kushuhudia makabidhiano ya bastola kwenda kwa CRO Dar es Salaam.

## Samia: Nadra kumpata mtu kama Maalim Seif

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezindua Taasisi ya Maalim Seif, akisema ni nadra kumpata mtu mwenye haiba ya mwanasiasa huyo kwa kuwa amefanya kazi kubwa ya mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kiutawala Zanzibar.

Uzinduzi huyo ulifanyika jana katika Hoteli ya Golden Tulip pembezoni mwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Zanzibar, ukihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kiserikali, vyama vya siasa na asasi za kiraia.

Rais Samia alisema Maalim Seif alikuwa makutano ya watu na kiongozi wa watu na ndio maana watu wakamshiba katika mioyo yao.

Alisema uimara wake, utu wake, fikra zake, uthabiti wa kauli zake, utajiri wa moyo wake ni kati ya mambo mengi yaliyofanya watu kumpenda na kumheshimu Maalim Seif.

"Kwa sababu hiyo, alijijengea ufuasi mkubwa miongoni mwa watu, sio kwa madaraka au nafasi alizoshika bali ni aina ya maisha aliyoishi," Rais Samia alisifu.

Alisema Maalim Seif alifanya kazi ya ualimu na ualimu wake ni maalum kwa sababu alikuwa ni mwalimu wa watu na sio tu kwa wanafunzi darasani na ndio maana jina la Maalim lilimganda kama sehemu ya jina lake.

Alisema watu kama Maalim Seif ni nadra kutokea katika maisha, hivyo busara inahitajika kuhifadhi kumbukumbu zake kwa ajili ya kufaa vizazi vya sasa na vijavyo.

Alisema kiongozi huyo alikuwa thabiti kwa misimamo yake na utayari wake wa kutafuta maridhiano pale panapokuwa na misuguano na kutofautiana katika jambo analoliamini na aliifanya kazi hiyo ndani na nje ya chama chake.

"Hii sio sifa ya kawaida kwa wanasiasa na viongozi duniani, mtakubaliana na mimi mara nyingi hasa katika nchi zinazoendelea wanasiasa wakitofautiana kinachofuata ni vurugu, lakini akiwapo mtu kama Maalim Seif vurugu hukatika na maridhiano yakaendelea.

"Sisi tunaomfahamu Maalim Seif pale anapokuwa na misimamo tofauti, hakusita kujipambanua nao ingawa alikuwa tayari kuzungumza, alikuwa akipambana kwa hoja bila ya kumtusi mtu, wala kugombana na mtu, hakuogopa gharama za kusimamia anachokiamini na Maalim Seif aliendelea kuwa yule yule," alisema.

Alikumbusha kuwa Maalim Seif alikuwa mstari wa mbele kupigania kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi mnamo mwaka 1989 mpaka 1992.

"Maalim Seif alishiriki na kufanikisha maridhiano baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, utayari wake wa kuangalia maslahi mapana ya kitaifa ndiyo yaliofanikisha chama cha CCM na ACT-Wazalendo kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na yeye kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa kweli amefanya kazi kubwa," Rais Samia alisifu.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema Maalim Seif ana historia ndefu katika medani za siasa Tanzania na amekuwa sehemu ya siasa na uongozi nchini kwa zaidi ya miaka 45 ya kutumikia nafasi mbalimbali za uongozi kutoka CCM, CUF na ACT-Wazalendo.

## HABARI KITAIFA

# Maagizo matatu ya Bunge tishio la njaa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali mambo matatu ya kufanya ili kukabiliana na baa la njaa na mfumuko wa bei ya vyakula unaoweza kutokea mwakani baada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutabiri kuwapo kwa uhaba wa mvua kwa msimu wa mwaka 2021/22.

Septemba mwaka huu, TMA ilitoa utabiri unaoeleza kwamba mvua za vuli zinazotarajiwa zitakuwa chini ya wastani na huenda zikasababisha sehemu kubwa ya mikoa inayopata mvua hizo kwa misimu miwili kwa mwaka kuwa na ukame.

Pia ilitabiri kutakuwa na vipindi vya joto kali kuliko kawaida katika msimu wa vuli huku ikitaja mikoa itakayopata mvua ya wastani na chini ya wastani kuwa ni Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Simiyu, Mara, mashariki mwa Mkoa wa Shinyanga na visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia.

Mikoa mingine iliyotajwa ni ya Kanda ya Ziwa, ikiwamo Kagera, Geita, Mwanza na kaskazini mwa Kigoma ambayo itapata mvua za wastani na chini ya wastani.

Kutokana na hali hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Sillo Baran, akiwasilisha taarifa ya kamati hiyo kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/23, pamoja na mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23, alisema kamati inaishauri serikali kuendelea kujenga vihenge na maghala ya kuhifadhia nafaka kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa chakula nchini kuliko ilivyo hivi sasa. Alisema: "NFRA wana uwezo wa kuhifadhi tani 501,000 tu. Kwa hali hii ina maana kwamba hata serikali ikiendelea kuipa NFRA fedha za ununuzi wa nafaka, uwezo wake wa kuhifadhi ni asilimia 36 ya ziada ya nafaka iliyozalishwa katika msimu wa mwaka 2020/21."

Baran alitaja ushauri mwingine ni serikali kuendelea kuiwezesha kifedha NFRA ili iwe na uwezo wa kununua ziada ya chakula, kuleta uhimilivu wa bei inapotokea njaa na kuuza nje ya nchi pindi taifa linapokuwa limejitosheleza.

Alisema serikali inapaswa kuiwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) kimtaji ili itekeleze majukumu yake ya kununua mazao na kuyauza kibiashara pale ambapo uwezo wa NFRA kuhifadhi mazao unapokuwa mdogo.

Kadhalika, alisema tathmini ya awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula msimu wa mwaka 2020/21 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2021/22 imeonesha kuwa hali ya uzalishaji wa chakula inatarajiwa kufikia kiasi cha tani 18,425,250 mwaka 2020/21 kwa mlinganisho wa nafaka, kulinganishwa na tani 18,196,733 msimu wa 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Alifafanua kuwa mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/22 yanakadiriwa kuwa kiasi cha tani 14,796,751, kwamba tani 9,417,888 ni mazao ya nafaka na tani 5,378,864 ni mazao yasiyo nafaka.

Alisema nchi inategemewa kuwa na ziada ya tani 3,628,499 za chakula, kwamba tani 1,222,103 ni mazao ya nafaka na tani 2,406,396 ni mazao yasiyo nafaka.

Hata hivyo, Baran alisema TMA imetabiri kuwapo kwa uhaba wa mvua kwa msimu wa mwaka 2021/22 unaoweza kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula kwa mwaka 2022/23 na hivyo kusababisha mfumuko wa bei za vyakula nchini.

# Masharti mafao waliofutwa kazi uhakiki wa vyeti 2017

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amesema msamaha wa kuwalipa mafao na kuwarejesha kazini walioutoa, hauwahusu watumishi walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti au kutoa taarifa za uongo katika kumbukumbu zao rasmi za kiutumishi kuwa wana elimu ya kidato cha nne.

Akitoa ufafanuzi huo jana jijini Arusha, Waziri Mchengerwa, alisema ameita vyombo vya habari kuujulisha umma juu ya suala hilo ili waondokane na upotoshaji na mijadala inayoendelea kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari.

Alisema msimamo wa serikali ni kwamba watumishi wote 15,538 waliobainika kughushi vyeti hadi sasa, hawastahili kurudishwa kazini wala kulipwa malipo yoyote.

Alikumbusha kuwa mwaka 2004, serikali ilitoa waraka uliobainisha watumishi wote watakaoajiriwa kuanzia Mei 20, 2004 wanatakiwa kuwa na elimu ya kidato cha nne ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Ajira na Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na kanuni za utumishi wa umma.

"Katika utekelezaji wa matakwa hayo mwaka 2017 wakati wa zoezi la uhakiki wa vyeti na watumishi hewa, ilibainika baadhi ya watumishi wenye elimu ya darasa la saba waliajiriwa bila kuwa na cheti cha ufaulu wa elimu ya kidato cha nne," alisema.

Alisema hivyo watumishi hao waliondolewa kazini kutokana na kukosa sifa kwa mujibu wa miundo ya utumishi ya kada zao.

Alisema katika zoezi hilo baadhi ya waajiri waliwaondoa kwenye orodha ya malipo ya mishahara kimakosa watumishi wasiokuwa na elimu ya kidato cha nne walioajiriwa kabla ya Mei 20 mwaka 2004.

"Kutokana na makosa hayo mwaka 2018 serikali kupitia waajiri na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliwarejesha kazini na kuendelea kuwalipa mishahara jumla ya watumishi 4,380 walioondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara kimakosa.

"Idadi hii ina jumuisha watemdaji wa kata, watendaji wa mtaa na watendaji wa vijiji wapatao 3,114," alifafanua.

Alisema pamoja na kuwarejesha watumishi hao pia serikali ilitoa msamaha wa kuwarejesha kazini watumishi walioondolewa kazini kwa kukosa sifa ya elimu ya kidato cha nne na baadaye wakajiendeleza na kupata sifa tajwa hadi ifikapo Desemba mwaka jana.

Alisema msamaha huo uliwahusu watumishi waliojipatia vyeti vya elimu ya kidato cha nne ambao hawakudanganya katika taarifa zao kuwa wana elimu ya kidato cha nne na wale wasiobainika kughushi vyeti.

Alisema pamoja na jitihada za serikali hapakuwa na utaratibu bayana wa kushughulikia haki na stahiki za watumishi walioondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara kwa kuajiriwa bila kuwa na cheti cha ufaulu wa elimu ya kidato cha nne.

"Kutokana na ombwe hilo, Rais Samia Suluhu Hassan, alielekeza watumishi wote walioondolewa kwa kukosa sifa ya kuwa na elimu ya kidato cha nne wapatiwe stahiki zao na waajiri wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA YA UTENGENEZAJI, UPIMAJI, USAMBAZAJI NA UTOAJI WA MABOMBA MAKUBWA YA HDPE**
**KUMBUKUMBU 0010007214**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya HDPE Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP inahitaji huduma za mtengenezaji mwenye uzoefu na mwenye sifa nzuri kutoa huduma za utengenezaji, upimaji, usambazaji na utoaji wa mabomba makubwa ya ukuta wa HDPE kulingana na viwango na vipimo vilivyotajwa hapa chini:

**VIWANGO:**

Ukuta wa muundo wa Bomba za HDPE zitalingana kwa kuzingatia viwango EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake, isipokuwa ikiwa imeainishwa vinginevyo.

**VIPIMO:**

- Kuta za kila sehemu ya HDPE (2.45m) zitalingana na vipimo vifuatavyo.
- ID / DN1500 na kipenyo ch nje cha ukubwa 1630 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- ID / DN1800 na kipenyo cha nje cha ukubwa 1960 ± 10mm takriban idadi ya mita 400+ zinatakazowasilishwa katika sekesheni za mita 2.45.
- KAMPUNI ina haki ya kuthibitisha utengenezaji wa mabomba ya HDPE yaliyowekwa katika kiwanda cha uzalishaji cha Mtengenezaji kulingana na mfumo wa usimamizi wa ubora kulingana na ISO 9001: 2015. Mfumo wa usimamizi wa ubora wa mtengenezaji utahitatakika kuwa uliothibitishwa kwa ISO 9001: 2015 na chombo cha uthibitisho cha Kimataifa.
- Malighafi inayotumika kutengeneza ukuta wa muundo wa bomba za HDPE na viunganishi vyake lazima vilingane na EN13476-1 / ISO 21138-1. Mahitaji ya ubora wa Bomba za HDPE na upimaji wao ni utahitajika kulingana na viwango EN13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake husika. Mahitaji ya ubora wa viunganishi zilizotengenezwa kutoka kwa muundo wa bomba za HDPE zitahitajika kulingana na EN 13476-2 / ISO 21138-2, na marekebisho yake ya hivi karibuni.
- Mabomba yote ya HDPE yaliyotengenezwa kwa ukuta yatakayotolewa dhidi ya Zabuni hii "yatatiwa alama" kulingana na viwango vya sahihi vinavyotumika.
- Kwa ombi, nyaraka za ubora wa bidhaa zinazotolewa zinapaswa kuwasilishwa na mtengenezaji kupitia vyeti vya kufanya kazi kulingana na viwango vinavyotumika. Rekodi zote za matokeo ya vipimo vya ubora zitahifadhiwa na mtengenezaji kwa marejeleo yajayo.

- Kabla na baada ya kutoa zabuni kwa Mtengenezaji, KAMPUNI ina haki ya kukagua uwezo wa upimaji na kushuhudia majaribio yaliyofanywa katika kituo cha Maabara cha Mtengenezaji kutathmini ubora wa bidhaa kulingana na viwango vinavyotumika. KAMPUNI itateua mwakilishi kushuhudia majaribio yote yaliyofanywa katika kituo cha maabara cha Mtengenezaji na mwakilishi atawasilisha matokeo yote ya mkandarasi/mzabuni husika & KAMPUNI kwa kujitegemea. KAMPUNI ina haki ya kuidhinisha Bidhaa kulingana na ripoti za majaribio ya ubora kabla ya kupelekwa kwenye eneo la ujenzi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa chini ya upeo wa kazi, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 15 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:

  Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa yo miundombinu nchini Tanzania.
- Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
- Kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.

Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.

Taasisi zenye nia na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kuwasilisha nia kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **09 Novemba 2021.**Kichwa cha Habari cha Barua Pepe kiwe ni **0010007214.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216553602

## Shahidi kesi Sabaya adai hakwenda PCCB kukamilisha upelelezi

**Na Allan Isack, ARUSHA**

OFISA TEHAMA wa Benki ya CRDB, Kanda ya Kaskazini, Geofrey Nnko (31), amedai kuwa Mei 31, mwaka huu, hakufika kwenye ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Arusha kujaza fomu namba 28 na 29 za kuruhusu kutolewa kwa video zilizochukuliwa kwenye mfumo wa NVR unaomilikiwa na benki hiyo.

Shahidi huyo wa saba wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya na wenzake, amedai fomu hiyo alijaza akiwa katika benki hiyo Tawi la kwa Morombo jijini Arusha.

Katika kesi hiyo, mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanaokabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi.

Nnko alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alidai kwamba Mei 31 alikuwapo ofisini na alipewa agizo la kwenda katika tawi la benki hiyo la kwa Morombo jijini Arusha.

"Nilipewa taarifa na mkuu wangu wa kazi na nilikwenda katika eneo husika nililoagizwa," alidai shahidi.

Alidai kwamba hakuwahi kwenda ofisi za TAKUKURU bali alijaza fomu namba 28 na 29 akiwa katika tawi la benki hiyo la Kwa Murombo.

"Fomu hii na maelezo yake inaonyesha kwamba nilisaini nikiwa Kwa Murombo," alidai shahidi.

Vilevile shahidi huyo alidai mahakamani huko kwamba alichokitoa kwenye mfumo ni video zilizokuwa katika mpangilio wa chaneli na haikuwa kama ripoti.

"Nilimpatia Jonson Kisaka, ofisa wa TAKUKURU, flash ambayo ilikuwa na video ambazo zilikuwa kwenye mpangilio wa chaneli na siyo ripoti," alidai.

Shahidi alidai kwamba kama kuna uhitaji wa kutoa taarifa kutoka kwenye mifumo ya benki, kuna utaratibu wa kibenki wa kufuatwa ikiwamo kuwasiliana na mkuu wake wa kazi na kuonana na meneja wa benki tawi husika.

Alidai kuwa Mei 31, mwaka huu, alipokea taarifa kutoka kwa mkuu wake wa kazi akimtaka kufika tawi la benki la Kwa Murombo ili kutoa video iliyorekodiwa kwenye kinasa picha (CCTV camera).

Shahidi huyo alidai kwamba wakati wa mchatako wa kutoa video hizo, kamera na flash zilikuwa salama na hazikuwa na tatizo lolote.

# Serikali yarejesha tozo maegesho kielektroniki

**Na Mary Geofrey**

MFUMO wa ukusanyaji tozo za maegesho ya magari kwa njia ya kielektroniki umerejeshwa kuanzia Desemba Mosi, mwaka huu kwa masharti sita, ikiwamo kutotoza magari yaliyo nje ya nyumba za ibada. Vilevile, serikali inatarajia kuyafuta madeni yote ya maegesho yaliyoorodheshwa katika mfumo wa ukusanyaji kwa njia ya kielektroniki kabla ya mfumo huo kusitishwa Oktoba 9, mwaka huu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alitangaza utaratibu huo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu namna mfumo huo utakavyofanya kazi. Alisema waliamua kuusitisha baada ya kutokea kwa malalamiko ambayo kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara na Mijini na Vijijini (TARURA), wameyafanyia kazi na kuja na mfumo rafiki kwa wananchi wote. "Mfumo huu utaanza kazi rasmi Desemba Mosi, lakini baada ya TARURA kutoa elimu ya kutosha kwa jamii ndani ya 21 kuanzia Jumatatu Novemba 8 mwaka huu ili wananchi wapate elimu ya namna utakavyokuwa ukifanya kazi," alisema Ummy.

Waziri huyo alifafanua kuwa, katika maeneo ya nyumba za ibada hawatakiwi kutoza ushuru pamoja na magari ya kubeba wagonjwa.

Alisema gharama za kuegesha magari kwa saa moja ni Sh. 500 na kwa siku ni Sh. 2,500 kutoka 4,500 iliyokuwa inatozwa awali kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Alisema kwa Jiji la Mwanza na Arusha malipo ni Sh. 500 kwa saa na Sh. 1,500 kwa siku na kwa manispaa zote na majiji mengine malipo yatakuwa Sh. 500 kwa saa na Sh. 1,000 kwa siku. Halmashauri za miji malipo yatakuwa Sh. 500 kwa siku.

"Viwango hivi vimezingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhitaji mkubwa wa maeneo ya maegesho ya magari katika mji husika. Aidha, vimezingatia kutoa fursa kwa wananchi kuwa na uhuru wa kuegesha na kulipia kwa saa au kwa siku," alisema Ummy.

Kuhusu muda wa kulipa, Ummy alisema mtumiaji anapaswa kulipa ndani ya siku 14 tofauti na awali ilikuwa ndani ya siku saba.

Kuhusu adhabu, alisema wamefuta adhabu ya kuongeza mara mbili ya deni endapo atashindwa kulipa ndani ya siku saba na badala yake atalipa faini ya Sh. 10,000 badala ya Sh. 30,000 ya awali.

"Nimeelekeza wataalamu wangu kuhakiki madeni yote ambayo ni zaidi ya Sh. milioni 800 yaliyozalishwa wakati wa utekelezaji wa mfumo huo (Termis) na kuwasilisha kwenye mamlaka husika maombi ya kufuta madeni yenye changamoto zilizotokana na matumizi ya mfumo kuanzia siku ambayo mfumo ulianza kutumika," alifafanua.

Ummy alisema vikwazo vya baadhi ya wateja kushindwa kulipa kwa kukosa kumbukumbu namba, mfumo umeboresha na itatoka ndani ya dakika moja kwa njia ya kutolewa ankara. Alitaja njia zitakazotumika kukusanyia ushuru huo ni kwa kutumia TeRMIS App, GePG Tanzania, simu ya kawaida kwa kubonyeza *152*00# kisha kufuata maelekezo au wavuti ya mfumo inayopatikana kwa www.termis.tarura.go.tz

Alisema mfumo huo umesaidia kukusanya mapato kutoka Sh. milioni 25 hadi kufika Sh. milioni 40 kwa siku, akisisitiza: "Fedha nyingi zilikuwa zinaishia kwenye mifuko ya watu."



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, akipata nyama choma na wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wa eneo la Mchafukoge mapema wiki hii, alipotembelea eneo hilo kwa ajili ya kukagua miundombinu ya masoko yaliyotengwa kwa ajili yao. **PICHA: NEEMA EMANNUEL**

# Serikali yaanika athari mabadiliko ya tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** GLASGOW

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Selemani Jafo, amesema athari za mabadiliko ya tabianchi zinaonekana dhahiri katika maeneo mbalimbali nchini, akisisitiza ipo haja ya kuongeza jitihada za dhati katika kukabiliana nayo.

Jafo aliyasema hayo jana mjini Glasgow, Scotland katika mkutano wa 26 wa Nchi wa Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

Alizitaja athari hizo kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari kulikosababisha kisiwa cha Maziwe Wilaya ya Pangani na kisiwa cha Fungu la Nyani Wilaya ya Rufiji kumezwa na maji ya bahari na kuongezeka kwa kina cha maji kwenye Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika.

"Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi ili kukabiliana na athari hizi ambazo zinatishia kurudisha nyuma juhudi za serikali za miongo kadhaa za kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa watu wake," Jafo alisisitiza. Alisema kuwa katika mkutano unaoendelea, viongozi wa mataifa makubwa ambayo kwa kiasi kikubwa mataifa yao ndio chanzo cha uzalishaji wa hewa ya ukaa wameonyesha nia ya dhati ya kutekeleza makubaliano waliojiwekea ya kutoa fedha kwa wakati ili kutekeleza miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mataifa hayo yanawajibika kutokana na makubaliano ya Mkataba wa Paris ambao unazitaka nchi zilizoendelea kutoa kiasi cha Dola bilioni 100 kila mwaka kwa nchi zinazoendelea ili ziweze kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Tunadhamiria na kusisitiza kuwa sasa tutoke kwenye maneno na twende kwenye vitendo, wenye jukumu la kutoa fedha watoe ili miradi mbalimbali ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi iweze kutekelezeka kwa wakati," Jafo alisisitiza.

Waziri huyo alisema katika kuungana na Jumuiya ya Kimataifa kupunguza uzalishaji wa gesijoto, Tanzania pia imechukua hatua stahiki zikiwamo za kuandaa Mpango wa Taifa wa Kupunguza Gesijoto (2021-2026); kuimarisha usimamizi wa misitu na programu za upandaji miti; kuendelea na ujenzi wa mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere; ujenzi wa reli ya kisasa; kuanza kutumika kwa gesi majumbani na kwenye uendeshaji wa mitambo viwandani na kwenye magari badala ya dizeli na petroli na mfumo wa usafiri wa mabasi yaendayo kasi katika Jiji la Dar es Salaam ambavyo vinachangia kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa kwanza Rais (Zanzibar) Dk. Saada Mkuya, alisema athari za mabadiliko ya tabianchi ni kubwa kwa upande wa Zanzibar kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari na kusabisha baadhi ya visiwa kutoweka na baadhi ya maeneo ya ardhi kuingiwa na maji chumvi na kuathiri shughuli za uzalishaji hususan kilimo na uvuvi, hivyo kuathiri uchumi.

Awali Jafo na Dk. Saada walikutana na kufanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani Prof. Petteri Taalas na kuzungumzia masuala ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi ambayo ni kikwazo kikubwa kwa sasa duniani. Mkutano wa 26 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unaendelea Glasgow, Scotland na utamalizika Novemba 12 mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Ataka mapendekezo kuinua sekta ya bima

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, ameagiza menejimenti ya mamlaka ya bima na wafanyakazi kwa kushirikiana na wadau kuchambua kwa kina mahitaji ya msingi ya sekta hiyo na kuwasilisha mapendekezo yake serikalini kwa hatua stahiki za kisera na kisheria.

Aliagiza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Tutuba alisema kwa sasa matatizo katika sekta ya bima ni uwezo mdogo wa soko la ndani la bima kuhimili vihatarishi bila kushirikisha soko la nje.

"Kama wataalamu tujiulize ni namna gani nzuri ya kupunguza kiwango cha bima mtawanyo kinachokwenda nje, hili serikali imelimba sana, ni wakati sasa wa kuja na suluhisho, si maneno.

"Serikali inatambua umuhimu wa sekta ya bima katika uchumi wa maendeleo ya watu. Hata hivyo, kuna udhaifu katika eneo la mchango wa hii sekta kwenye pato la taifa kama nilivyoeleza hapo awali," alisema.

Kiongozi huyo aliwakumbusha kuwa nguvu kubwa inapaswa kuelekezwa kwenye eneo la kuwafikia wasiofikiwa.

"Menejimenti ya TIRA, wafanyakazi pamoja na wadau mnatakiwa kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma, mtakubaliana nami kwamba sekta hii kuwa dumavu kunasababishwa na ushiriki mdogo wa watu au umma kwenye shughuli za bima, kwa sababu wengi wetu hatuna elimu ya kutosha ya masuala ya bima," alisema.

Pia aliwaahidi kuwa wizara yake imeyachukua yote waliyoyaeleza ambayo wametaka wizara hiyo iingilie kati ili kukuza huduma za sekta ya bima hususani suala la kuidhinishwa kwa Sera ya Bima ya Taifa na kupatikana kwa bodi.

Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Mussa Juma alisema mkutano huo umelenga kuangalia shughuli za taasisi, kujipima wamefikia wapi na mikakati ya mwaka ujao.

"Kutokuwapo wa sera ya bima ya taifa ni kunatuathiri, sera ya bima ya taifa inatoa dira au mwongozo wa masuala yote ya bima nchini, inapokuwapo ndiyo sheria na mikakati inatengenezwa," alisema.

Aliongeza kuwa wakati mwingine wamejikuta wanakuwa na miongozo ambayo inaterereka kwa sababu sera haijawa tayari.



Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Joseph Sokoine (kulia), akizungumza na Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), Bard Vegar Solhjell, katika ofisi ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam jana. Katika mazungumzo hayo, walikubaliana kuimarisha ushirikiano katika sekta za nishati, utunzaji wa mazingira na matumizi bora ya ardhi. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Naibu Waziri azionya kampuni kwa kuchelewesha urasmishaji makazi

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezionya baadhi ya kampuni za urasmishaji makazi holela Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuchelewesha kazi huku zikiwatuhumu watendaji wa sekta ya ardhi kuwa ndio chanzo.

Mabula alitoa onyo hilo na kueleza kutoridhishwa na utendaji wa kampuni hizo baada ya mfumo kuonyesha kuwa kampuni hizo ndizo chanzo cha kuchelewesha urasmishaji makazi.

Katika kikao chake na watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri ya Manispaa ya Ubungo pamoja na kampuni hizo jana, kampuni hizo zilimweleza Naibu Waziri kuwa zinashindwa kukamilisha kazi kwa wakati kutokana na watendaji wa ardhi kushindwa kutoa kazi za upimaji wanazopeleka ofisi za ardhi kwa wakati.

Kutokana na tuhuma hizo, Dk. Mabula alizitaka kampuni hizo kufika ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam kuangalia mfumo wa miamala ya ardhi kwa lengo la kubaini wanaokwamisha kazi ili kuchukua hatua.

Hata hivyo, wakati wa kupitia kazi za kampuni kwenye mfumo, juzi ilibainika kuwapo uzembe kwa baadhi ya kampuni kwa kushindwa kufuatilia kazi zao au kutokuwa na mawasiliano na watu wanaowatuma kufuatilia kazi zilizopelekwa wizarani.

"Mfumo wa sasa hivi haudanganyi kabisa na ardhi ya sasa siyo ile ya zamani. Hata mtu akifanya vurugu ama kutegea kufanya kazi atagundulika tu kwa kuwa kila kitu kiko katika mfumo. Ninyi taarifa mmepewa tangu mwezi wa sita halafu mnailaumu wizara," alisema Dk. Mabula.

Naibu Waziri aliwaeleza wawakilishi wa kampuni za Dimwe Land Consult Ltd na Mosaik Company Ltd zilizofika ofisini kwa kamishna kuwa: "Sasa hivi ukitaka kufuatilia kazi za ardhi kupitia mfumo kuanzia mwanzo hadi mwisho utaipata na utagundua uzembe uko kwa mtendaji gani. Kwa sasa hakuna tena udanganyifu kama ilivyokuwa ikifanyika zamani."

Awali, katika ziara yake, Dk. Mabula alikagua mfumo unganishi wa taarifa za ardhi katika ofisi ya ardhi Manispaa ya Ubungo na kujionea utendaji kazi pamoja na changamoto zinazowakabili watendaji wa sekta ya ardhi, hivyo kuwataka kuongeza kasi ya utoaji hati za ardhi.

Aidha, Naibu Waziri alizungumza na wakazi wa Mbezi kwa Yusufu kwa lengo la kujua changamoto zinazowakabili kuhusiana na sekta ya ardhi sambamba na kutoa hati kwa wananchi waliorasimishiwa makazi.

Katika mkutano huo, wananchi wengi walilalamikia kampuni za urasmishaji makazi holela kwa kuchelewesha kazi huku zikiwa zimechukua fedha za wananchi .

# Mwitikio waonekana kuchanja UVIKO-19

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Hospitali Kuu ya Kijeshi Lugalo, Brigedia Jenerali Fredi Kivamba, amesema kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wafanyakazi kada ya jeshi kujitokeza kupata chanjo ya Uviko-19.

Brigedia Jenerali Kivamba aliyasema hayo mkoani Dar es Salaam wakati akihojiwa na waandishi wa habari katika mahafali ya kozi za stashahada ya Ofisa Tabibu kundi la 15 na stashahada ya Ofisa Uuguzi na Ukunga kundi la 18 waliohitimu jana katika Chuo cha Kijeshi cha Sayansi za Tiba Lugalo.

"Moja ya sababu ya kada hii kuchangamkia chanjo ni kutokana na mataifa mbalimbali ya nje ya nchi ambayo moja ya masharti yaliyoweka ili watu waweze kuingia katika nchi zao lazima wawe wamepata chanjo ya Uviko-19," alisema.

Alikumbusha kuwa chanjo ni hiari na wanajeshi wao wakitaka kwenda nchi zingine ni lazima wachanje, hivyo wameendelea kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kupata chanjo ili kujikinga na Uviko-19.

Alisema wahitimu hao wanapomaliza kozi hizo wanakwenda kusaidia jamii katika hospitali mbalimbali nchini.

Alisema japokuwa ni chuo cha kijeshi, kipo huru kwa ajili ya kusaidia umma wa Watanzania kwa kuwa wanatibu bila kuwa na mipaka, hivyo asilimia 80 ya wanaotibiwa katika hospitali hiyo ni raia wa kawaida.

Akizungumzia tabia za ukosefu wa maadili ya kazi kwa wahudumu wa afya, alisema hiyo ni tabia ya mtu kwa kuwa miiko ya kitabibu inafundisha jinsi ya kufanya kazi kwa uadilifu na inapotokea hali ya ukosefu wa maadili, bodi ya matibabu inachukua hatua dhidi ya mhusika.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho cha Kijeshi Lugalo, Luteni Kanali Sisco Kalongola, aliwataka wahitimu waliomaliza kufanya kazi kwa bidii ikiwa ni pamoja na kujiendeleza zaidi kielimu.

Alisema kwa mwaka mpya wa masomo wa 2021/22 chuo hicho kimeongeza kozi moja ya stashahada ya ofisa tabibu meno na kinywa ambayo imeanza ikiwa na wanafunzi 18.

Alisema chuo hicho kilianzishwa mwaka 1982 chini ya Hospitali Kuu ya Jeshi na mwaka 2015 kilijitenga na kuwa chuo kamili na kuitwa Chuo cha Kijeshi cha Sayansi za Tiba.

Alisema wanafunzi 84 wamehitimu kozi ya maofisa tabibu na uuguzi na ukunga ambao ni sawa na asilimia 78.5 na wengine 23 hawakuweza kuhudhuria mahafali hiyo kutokana na sababu mbalimbali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Riadha, kikapu, netiboli, bendera ya nchi inawadai

**WAKATI** kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kikiwa katika nafasi nzuri kwenye mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia zitakazochezwa Qatar mwakani, wanamichezo wa michezo mingine nao wanatakiwa 'kuamka'.

Kwa sasa Taifa Stars ambayo Novemba 11, mwaka huu itashuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwakaribisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na baadaye kuwafuata Madagascar nyumbani kwao, inaonekana inaweza kupata mafanikio ambayo haijawahi kupata hata mara moja.

Mashindano makubwa ambayo Taifa Stars imefanikiwa kushiriki ni Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), mara ya kwanza ilienda mwaka 1980 na mara ya mwisho ilikuwa ni 2019, fainali hizo zikichezwa nchini Misri.

Michuano mingine mikubwa ambayo timu hiyo imeshiriki ni Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), nayo imeshiriki mara mbili, mwaka 2008 ikiwa na Mbrazil Marcio Maximo na mwaka juzi ilipoongozwa na Mrundi Etienne Ndayiragije.

Hata hivyo safari ya Taifa Stars kuelekea Qatar bado inahitaji nguvu zaidi, lakini mafanikio ambayo yamefikiwa hadi sasa yanatakiwa kupongezwa ili kuwafanya wachezaji waendelee kupambana na hatimaye kufikia malengo ambayo nchi inayasubiri.

Endapo Stars itakata tiketi ya kushiriki fainali hizo, sio tu itaipa heshima nchi, lakini ikumbukwe itawafungulia pia 'milango' ya ajira kwenye klabu za mataifa yaliyoendelea kwa sababu mawakala kutoka sehemu mbalimbali wanatarajiwa kuwapo kusaka vipaji vya wachezaji kutoka Afrika.

Kwa njia ile ile, sasa huu ni wakati wa kuona wanamichezo wengine wanaongeza juhudi katika mashindano yao ya ndani na hatimaye kupata vikosi au wawakilishi imara ambao watakwenda kwenye michuano ya kimataifa wakiwa washindani.

Pazia la mashindano ya Taifa ya mpira wa kikapu linatarajiwa kufunguliwa wikendi hii jijini Dodoma, ni mashindano ambayo yanafanyika kwa mujibu wa kalenda yao lakini yanatakiwa kutoa nyota ambao wataiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Afrika Mashariki na baadaye Afrika.

Kikapu ni mchezo ambao unaweza pia kulitangaza vyema taifa kama wachezaji wake wataandaliwa vizuri na kufahamu umuhimu wa kubeba bendera ya Tanzania wanapokuwa wanashindana na wenzao kutoka mataifa mengine.

Hapo nyuma mchezo huo ulionekana ni wa wachezaji 'mabishoo' au watoto wa mjini kama vile wanaocheza kriketi au gofu walionekana ni wale wanaotoka katika familia zenye uwezo, la hasha, michezo hiyo iko huru na mchezaji wa aina yoyote anaruhusiwa kucheza.


Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na serikali yake amekuwa shabiki namba moja wa michezo yote, katika utawala wake anataka kuona kila mchezo unafanya vizuri katika ngazi ya ndani na nje ya nchi, amekuwa karibu na wanamichezo wote ili kuhakikisha nchi inafanya vyema na kutokuwa wasindikizaji.

Tunawakumbusha michezo ni ajira na kufanya vizuri kwa timu zetu kwenye mashindano ya kimataifa, si tu kutailetea nchi sifa, lakini kikubwa kitafungua milango ya wadhamini na hapo suala la ukata litasahaulika kuanzia kwenye kambi hadi maandalizi ya safari.

Ni matarajio ya kila mmoja wetu kuona ndoto zake zinafikiwa, hivyo kwa sasa ni matarajio ya Rais Samia kuona Tanzania inarejea kwenye makali yake katika kila mchezo na hii inatokana na uwekezaji na ushirikiano ambao upo kati ya serikali na viongozi wa vyama vya michezo yote hapa nchini.

Na katika kuonyesha pia Rais Samia hajawaacha wasanii, serikali ilikubali kuwa wenyeji wa mashindano ya Miss and Mr Viziwi ya Afrika huku pia ikikubali uteuzi wa kuwa mwenyeji wa mashindano hayo ya dunia yatakayofanyika mwaka 2023.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Muumba ndiye muumbua

Na Barnabas Maro

**MUNGU** ambaye huumba ndiye mwenye uwezo wa kuumba. Methali hii hutumiwa kumzindua mwanadamu aliyetawaliwa na hadaa au ghururi zinazotokana na uwezo wake na kuanza kujiona mwenye uwezo mkubwa na kuwatisha wenzake.

'Hadaa' ni tendo la kudanganya; kitendo cha kudanganya kwa hila; tendo la kumfanyia mtu udanganyifu;= hila. 'Ghururi' ni udanganyifu unaomsababisha mtu kutofanya mambo yenye manufaa naye.

"Bendera ipepeayo sana mwishowe huchanika." Maana yake bendera au beramu inayopepea sana mwishowe huchanika. Huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu anayejisifu na kujitangaza kwa uwezo alionao. Hatimaye uwezo huo utaisha na abakie katika hali duni au mbaya.

Aidha "Ushungu mwenda nao, shingo ujeze matama." Ushungu ni sumu, Ujeze ni amejaza, Matama ni funda la kitu kiowevu kama mate au uji. Maana yake anayekwenda na sumu (hasira) huwa amejaza mafunda shingoni mwake.

Huweza kutumiwa kupigia mfano mtu ambaye ana tabia ya kutumia lugha chafu ya ufidhuli kila aendako. Pia hutumiwa kuwanasihi watu dhidi ya kutumia lugha chafu kwa kuwa kwa njia hiyo watafanya wengine kuwachukia au kutowapenda.

Sambamba na hilo, "Asiyekiri ushinde (tendo la mtu la kukiri kushindwa) hakuwa mshindani." Maana yake mtu asiyekubali baada ya kushindwa si mshindani. Twanasihiwa tukubali tushindwapo au tukiri udhaifu wetu badala ya kutoa lawama zisizokuwa na msingi.

Baada ya Simba kutoka sare na 'ndugu zao' Coastal Union ya Tanga, dada fulani wa Simba alilalamika hadharani kuwa wapinzani wao wajadi ,Yanga, eti walihusika kwa kuwaroga ili washindwe na 'ndugu zao' waliojipa jina la Mmbwa mwitu! Eti wao (Simba) watalipiza kisasi kwa kutumia njia ile ile iliyotumiwa na Yanga ili nayo ishindwe!

Dada huyo wa Simba alimaliza viapo vyote kuwa wao kutofungana na Coastal Union, eti Yanga ilitia mkono wake yaani uchawi ili Simba ishindwe! Akaapa kuwa na wao watalipiza kisasi ili Yanga ifungwe!

Mechi iliyofuata ilikuwa Yanga dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam huku dada yule akijiapiza kuwa nao wangetia mkono ili Yanga ifungwe kwani wao ndiwo waliofanya hivyo hata Simba ikashindwa kuifunga Coastal Union!

Katika mahojiano na kituo kimoja cha redio nchini aliapa 'wachawi' wa Yanga waliingia uwanjani kuweka uchawi hivyo na wao watalipiza kisasi ili Yanga ifungwe na Ruvu Shooting. Badala yake, Yanga iliifunga Ruvu Shooting mabao 3-1. Sijui alijisikiaje kwa matukio yale!

Kwa upande mwingine, kunapokuwa na mechi , kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa au Uwanja wa Uhuru hasa zikutanapo Simba na Yanga huwa na ulinzi mkali usiku na mchana kuzuia wachawi kuweka takataka zao. Kwa ajili hiyo Simba na Yanga huwa na watu wao waitwao 'makomandoo' wanaolinda uwanja usiku na mchana kuzuia wachawi wasifanye mambo yao.

Biblia yatwambia ; "Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona , bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana aombaye hupokea, naye atafutaye huona, naye abishaye atafunguliwa. "Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akiomba mkate , atampa jiwe? Au akiomba samaki , atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi, mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je, si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni atawapa mema wao wamuombao?" (Mathayo 7-11.)

Hali ilivyo kwa Simba na Yanga ni kama jogoo wawili wasioweza kusaidiana kukamata kidudu. Maana yake jogoo wawili hawawezi kupatana na kusaidiana kukikamata kidudu kidogo.

Methali hii inatufahamisha kuwa watu wanaoshindana hawawezi kusaidiana wala kushirikiana kwa kufanya jambo hata kama ni dogo sana.

Ndo maana mara kwa mara hizi timu mbili maarufu nchini na Afrika Mashariki zatakiwa kutambua kuwa "waungwana hawagombani. Maana yake watu ambao ni waungwana hawagombani." Hutumiwa kutukumbusha kuwa ugomvi sio mzuri au haufai kwa waungwana.

Kumbe ndio maana wahenga walisema: "Adui wa mtu ni mtu." Maana yake binadamu huhasiriwa na binadamu mwenzake. Methali hii inatukumbusha kuwa aghalabu matatizo tuyapatayo husababishwa na watu tunaoishi nao kila siku.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 335 096.**

HABARI BUNGENI

# Serikali yasema hakuna ubia na sekta binafsi uendeshaji vyuo

BUNGE limeelezwa kuwa serikali kwa sasa haina utaratibu wa kushirikiana katika kutoa mafunzo ya ufundi na taasisi binafsi.

Hata hivyo, imesema inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi, zikiwemo taasisi za dini katika utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ludewa (CCM), Joseph Kamonga.

Mbunge huyo alihoji sababu za serikali kutoingia makubaliano na Chuo cha Ufundi Lugarawa kinachomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Njombe kwa kupeleka walimu, vifaa na fedha za ruzuku ili wana Ludewa na wana Njombe wapate mafunzo hapo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema serikali inaendelea kuimarisha taasisi zake za elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga vyuo katika ngazi za wilaya na mikoa na kuvipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuhakikisha Watanzania wanapata elimu bora ya ufundi karibu na maeneo wanayoishi. "Katika mkoa wa Njombe, serikali inamiliki Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Makete chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 160 kwa mwaka,"alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa serikali inaendelea kupanua chuo hicho kwa kuongeza madarasa matano yenye uwezo wa kubeba wanafunzi 100 kwa wakati mmoja, mabweni mawili yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 72 kwa kila moja na nyumba mbili za watumishi, kila moja ikiwa na uwezo wa kubeba familia mbili.

"Serikali pia inaendelea na matayarisho kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Njombe kitakachojengwa katika Wilaya ya Ludewa kupitia fedha za IMF (Shirika la Fedha Duniani) na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi huu,' alisema.



Mbunge wa Jimbo la Vunjo, Charles Kimei, akichangia hoja Bungeni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Marekebisho sheria TAZARA mbioni kukamilika

MCHAKATO wa kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) utaisha hivi karibuni baada ya serikali ya Zambia kukamilisha kazi inayoendelea ya uteuzi wa viongozi katika ngazi mbalimbali.

Pia kunatarajiwa kuwa na kikao cha pande zote mbili kwa ngazi ya makatibu wakuu na mawaziri cha kuridhia mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbeya Vijijini (CCM), Oran Njeza.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kugharamia matengenezo ya reli ya TAZARA ambayo miundombinu yake imechakaa na ni muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania na hata nchi jirani za SADC.

Waitara, akijibu swali hilo, alisema TAZARA ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya TAZARA namba 23 ya mwaka 1975 iliyorekebishwa kwa Sheria ya TAZARA namba nne ya mwaka 1995.

Alisema reli hiyo inamilikiwa kwa uwiano wa hisa hamsini kwa hamsini (50:50) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia.

Hata hivyo, alisema serikali ya Tanzania inatambua umuhimu wa kugharamia matengenezo ya reli ya TAZARA ndiyo maana inaendelea na jitihada za kukamilisha marekebisho ya sheria namba nne ya mwaka 1995 ambayo kukamilika kwake kutaondoa kero zinazoathiri uwekezaji katika reli hiyo kwa kuwa uwekezaji unaofanyika sasa hauongezi thamani ya hisa za nchi inayowekeza.

Pamoja na kuwapo kwa kero hiyo, alisema Serikali ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa TAZARA inaendelea kutoa huduma wakati jitihada za marekebisho ya Sheria zikiendelea.

"Kwa mfano, Katika bajeti ya mwaka 2017/18 Serikali ya Tanzania iliipatia TAZARA jumla ya Sh.Bilioni 10 kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya kutengenezea vichwa saba vya treni na vifaa vya kuongeza uwezo mgodi wa mawe na kiwanda cha kutengenezea mataruma ya zege vilivyoko Kongolo mkoani Mbeya,"alisema.

Pia alisema vipuri na mashine hizo vimeshanunuliwa na matengenezo ya injini yamekamilika mwaka 2020 na hivi sasa zinafanya kazi.

"Aidha, Serikali ya Tanzania inaendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi wa TAZARA upande wa Tanzania ambapo katika bajeti ya mwaka 2021//22 zimetengwa Sh.bilioni 14.98,"alisema.




**Na Augusta Njoji,** DODOMA

## Mbunge alia ubovu wa vituo vya afya jimboni

MBUNGE wa Bukene (CCM), Selemani Zedi, ameitaka serikali kujenga jengo la wodi za kulaza wagonjwa pamoja na kupeleka mashine ya X-ray katika Kituo cha Afya Itobo.

Akiuliza swali bungeni jana, Zedi alisema vituo vya afya vya zamani vikiwamo vya Itobo na Bukene, havina miundombinu inayofaa kuitwa kituo cha afya kutokana na kutokuwa na maabara, wodi wala chumba cha kufanyia upasuaji na X-ray.

"Tunahesabiwa kuwa na vituo vya afya lakini ukweli ni haviendani na vya sasa kutokana na kukosa miundombinu inayopaswa kuwapo,"alisema.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali imepeleka Sh. milioni 250 katika Kata ya Itobo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kituo hicho ili kuwa na uwezo wa kutoa huduma za upasuaji.

"Ujenzi wa majengo hayo umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo Aprili 30, 2022. Ujenzi wa vituo hivi vya afya unafanyika kwa awamu, hivyo baada ya awamu hii ya kwanza ya ujenzi kukamilika, serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine ikiwamo wodi katika Kituo Cha Afya Itobo,"alisema.

Aidha, alisema mashine za X-ray zitaendelea kununuliwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

"Serikali inatambua vituo vyetu hivi vina upungufu wa miundombinu na ujenzi huu ni wa awamu tunajenga kwasasa majengo ya kuanzia na awamu ya pili tutajenga wodi na majengo mengine,"alisema.

# Ufugaji samaki wafana JKT

Na Renatha Msungu, RUVU

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeanza ufugaji wa samaki katika Kikosi cha Ruvu JKT ambapo mpaka sasa lina vizimba 25 vyenye samaki zaidi ya 87,000.

Akizungumza na wandishi wa habari jana wakati wa ziara ya kutembelea katika vizimba hivyo vilivyopo Ruvu mkoani Pwani, Mkuu wa Tawi la Utawala wa Jeshi hilo, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema lengo lao ni kuja wanaongeza idadi ya ufugaji samaki ili kuongeza vizimba vya samaki.

Alisema samaki hao wanapatiwa chakula bora ili wakue kama ilivyotarajiwa ndio maana wanaonekana kuwa na afya nzuri katika vizimba hivyo.

"Tunaendelea na ufugaji wa samaki ili kuhakikisha tunakuwa walimu katika suala zima la ufugaji samaki," alitamba Brigedia Jenerali Mabena.

"Tumelazimika kuvuna samaki kabla ya muda ili kupunguza idadi kwa ajili ya kuwapa nafasi waliobaki waweze kuzaliana na kuwa na afya bora," alisema Brigedia Jenerali Mabena. Alifafanua zaidi ya kuwa vikwazo vinavyowakabili ni uhaba wa mvua ambapo walitarajia zitakuwa nyingi lakini imekuwa kinyume cha matarajio yao.

Hata hivyo, alisema wameweza kukabiliana na kikwazo hicho kwa kuhakikisha maji hayapotei na wamelamika kuwa na hifadhi za ziada za maji.

Alisema samaki hao ni kwa ajili ya kulisha vijana wa kujitolea JKT lakini mpango uliopo ni kuongeza idadi ya samaki ili uzalishaji utosheleze mahitaji ya vijana wanaochukuliwa kwa mujibu wa sheria na kuwauzia wananchi wengine.

Mtaalamu wa samaki katika kikosi hicho, Sajenti Maulid Heri, alisema mradi huo ulianza Machi mwaka huu wakiwa na vizimba 25 ambapo kila kizimba kina samaki 3,500.

Alisema tayari wameanza kuwavuna samaki hao na kulisha vijana na askari ndani ya kikosi hicho huku akisema wameanza kuwavuna mapema kwa sababu ya kikwazo cha mvua.

Alifafanua zaidi kuwa lengo lao ni kuwa na vizimba zaidi ya 100 ili wawe na samaki wengi zaidi kwa ajili ya kula na biashara.

Alifafanua zaidi ya kuwa awali walianza na vizimba 21 na hivi sasa wana vizimba 25 ambavyo vina samaki zaidi ya 87,000, wote ni samaki wakubwa.

Alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 134 na unatarajia kuingiza Sh. milioni 200 ndani ya miezi sita utakapoanza kutumika.

"Tunatarajia kupata Sh. milioni 200. Kwa hiyo faida ipo ndio maana tunasimamia vizuri samaki hao," alisema Sajenti Maulid.

Alisema wao wana ufugaji wa kisasa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ndio maana samaki hao wanakua kwa haraka na kwa kutumia teknolojia hiyo wameanza kuzalisha vifaranga vya samaki kwa ajili ya mbegu.



Ofisa Msimamizi Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Morgan Isdor (kushoto), akimuelekeza mlipakodi wa eneo la Majimoto, mkoani Katavi jana, kuhusu namna ya kuperuzi tovuti ya TRA na kupata huduma mbalimbali kwa njia ya mtandao kupitia simu janja yake, wakati wa kampeni inayoendelea ya elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango. **PICHA: TRA**

# Makamu wa Rais aonya upendeleo mahakamani

Na Gwamaka Alipipi

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewataka wadau wa mahakama kuwa chombo huru na kisicho na upendeleo ili wananchi waziamini taasisi za Mahakama Afrika.

Pia amezitaka taasisi hizo kuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya rushwa mahakamani na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwenye mahakama.

Aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa tano wa majadiliano ulioandaliwa na Umoja wa Mahakama za Afrika.

Alisema suala la mahakama kuwa chombo huru kisicho na upendeleo ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wanajenga uaminifu kwa chombo hicho.

"Kwa mfano Katiba ya Tanzania inatenganisha utendaji wa mihimili ambayo ni Mahakama, Bunge na Serikali na haviingiliani katika kazi zao," alisema Dk. Mpango.

Alifafanua kuwa pamoja na kwamba katiba hiyo humpa mamlaka Rais wa Tanzania kuteua majaji, lakini pindi wanapoteuliwa tu mikono ya Rais hufungwa na kumwacha jaji husika kufanya kazi zake kwa uhuru.

Dk. Mpango alisema: "Hatua hii imelenga kutoa uhuru kwa mahakama na kumwachia jaji afanye kazi yake bila upendeleo."

Alisema jambo lingine la kuwajengea uaminifu wananchi katika mahakama ni udhibiti wa rushwa ambao umekuwa ukiwalinda wahalifu, siyo tu mahakamani bali hata serikalini na kunyima haki wahusika.

Alisema ni wakati mwafaka kwa mahakama kubadilika na kuanza kutumia TEHAMA katika kuandaa, kuhifadhi nyaraka za mahakama na kusikiliza mashauri kupitia mikutano ya video jambo litakalokiweka chombo hicho karibu zaidi na wananchi.

"Kadri nilivyokuwa nasafiri sehemu mbalimbali nchini, ninakutana na vilio kutoka kwa wananchi kuhusu namna wananchi hawaridhishwi na utendaji wa mahakama kama vile kesi kuahirishwa kwa muda mrefu au kutosikilizwa kwa muda mrefu.

"Hii inaendana na msemo kwamba haki inayocheleweshwa ni sawa ana haki iliyonyimwa. Lakini pia nilikutana na vilio kuhusu gharama kubwa za kesi lakini pia uamuzi wa kesi kuandikwa kwa lugha za kigeni, unyanyapaa dhidi ya wanawake, watu wenye ulemavu na maskini," alisema Dk. Mpango.

Rais wa Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu, Imani Aboud, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuiunga mkono mahakama hiyo ikiwamo kuwa nchi mwenyeji wa mikutano yake.

## Mwingulu apewa kazi maalum TFA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Mchemba, anatarajiwa kuzindua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama cha Wakulima Tanganyika (TFA) unaofanyika leo katika Chuo cha Uhasibu jijini Mbeya.

TFA katika juhudi zake za makusudi za kuwahudumia wananchi na wakulima nchini, kimeandaa mkutano mkuu mahasusi kwa wakulima na wanahisa wake kutoka kote nchini.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Justine Shirima,

Mkurugenzi Mtendaji wa TFA, ilibainisha kuwa lengo la mkutano huo ni kuzileta pamoja kampuni za kimataifa ambazo zina uzoefu wa muda mrefu katika kuwahudumia wakulima kwa utaalamu wa hali ya juu ili kuzalisha mazao bora.

Alisema mkutano huo unajumuisha kampuni na washirika kutoka Marekani, Brazil, India, China na Ulaya.

"Pia utaleta mapinduzi makubwa ya kilimo katika usimamizi wa mbolea na udongo ambao kwa hakika utaongeza mavuno na mapato ya wakulima.

"Yote haya yataongeza ujuzi na uzoefu ambao jumuiya ya wakulima Tanzania na Afrika inakosa na hivyo tunatarajia kujenga ushirikiano imara kwa maendeleo ya kilimo chetu cha Tanzania.

"Ili kuhakikisha haya yote yanatokea, tuna washirika kutoka pande zote za dunia ambao wanatuunga mkono ili kufikia malengo haya makubwa," alisema.

Aliongeza kuwa sambamba na mkutano huo, wameanzisha bidhaa mpya ya mbolea 'TFA FAHARI' ambayo ni mbolea bora na halisi lakini pia inakidhi vyema hali ya udongo kwenye mashamba mengi nchini.

"Kumbukeni kuwa hivi karibuni tulizindua mpango wa kuchambua viwango vya udongo yaani 'soil PH' ili kuwawezesha wakulima kupunguza matumizi ya mbolea ya viwandani na kuchochea mbolea bora na halisi.

"Katika kuunga mkono Wizara ya Kilimo na serikali, tumejitolea kuifikia nchi nzima na mpaka sasa tuna mtandao wa usambazaji wa matawi zaidi ya 17 nchini ambao utawawezesha wakulima wa nchi hii kufikia kilimo chenye faida na endelevu," alisema.

**KUHUSU TFA**

TFA imekuwa mmoja wa wadau wakubwa na wenye ufanisi katika sekta ya kilimo nchini tangu ilipoanza shughuli zake Tanganyika mwaka 1935.

TFA ina wanachama zaidi ya 4,800 wanaowakilisha sehemu mbalimbali za jumuiya ya wakulima wa Tanzania.

TFA pia inajumuisha wamiliki wadogo na wakubwa wa biashara kutoka kwa wanavijiji hadi mashamba ya serikali, kutoka mashamba ya familia hadi vyama vya ushirika, TFA inawakilisha wakulima wa Tanzania na jumuiya zao.



# Washauriwa kutoa maoni sheria mtoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, amewataka wadau wa masuala ya watoto kutoa maoni katika maboresho ya Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 ili kuondokana na vikwazo vilivyopo.

Jingu alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha wadau hao kuhusu rasimu ya maboresho hayo.

Alisema maoni ya wadau hayo yatasaidia kuwa na sheria ili iendane na wakati na kusaidia kutatua vikwazo mbalimbali vilivyopo

"Tulisikia maoni yenu kuhusu Sheria ya Mtoto na. 21 ya mwaka 2009 na sasa tumewaita hapa kwa ajili ya kupokea maoni yenu kutokana na rasimu iliyoandaliwa ya marekebisho tupeni maoni yenu tupate Sheria iliyo bora," alisema.

Alisema kumekuwa kikwazo kubwa kwenye kusikilizwa kwa mashauri ya watoto kutokana na kukosekana na maofisa ustawi wa jamii ambapo ni lazima wawapo katika mashauri hayo hivyo kukwamisha na kukosekana kwa kutolewa haki kwa mtoto.

"Pale ambapo maofisa ustawi wa jamii hawatoshi katika Maeneo yetu kunakwamisha ufuatiliaji na utekelezaji wa masuala ya ustawi na haki za mtoto. Hivyo kunahitajika marekebisho ili kupata mbadala wa kutekeleza majukumu hayo pale ambapo ofisa ustawi wa jamii anakosekana," alisema.

Pia alisema inachelewesha au kukwamisha huduma za kuasili watoto, usajili na usimamizi wa vituo vya kulelea watoto mchana na makao ya watoto.

Naye Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, Mwanaisha Moyo, alisema kikao hicho kitasaidia kupata uelekeo mzuri katika kuhakikisha masuala ya haki na ustawi wa mtoto vinazingatiwa katika utekelezaji wa masuala mbalimbali kuhusu mtoto.

# Vyakula na vipodozi vya milioni 26 vyateketezwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Kati limeteketeza bidhaa za vyakula na vipodozi visivyo na ubora zenye thamani ya Sh. milioni 26.4

Mkaguzi TBS Kanda ya Kati, Domisiano Rutahala, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa wakati wa uteketezaji wa bidhaa hizo, alisema zimepatikana kwenye maeneo mbalimbali ya biashara.

Alisema maeneo hayo ni pamoja na maduka na migahawa, baa, hoteli na stoo katika halmashauri zote za mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora ambazo zinaunda kanda hiyo.

Kwa mujibu wa mkaguzi huyo, bidhaa zilizoteketezwa zimetokana na ukaguzi uliofanyika kwa nyakati tofauti kwenye maeneo tajwa kati ya Januari na Oktoba, mwaka huu.

"Jumla ya kilo 4,056,596 zenye thamani ya Sh. 26,448,500 zimeteketezwa, ikijumuisha bidhaa za chakula na vipodozi zilizoisha muda wa matumizi, zenye viambato sumu na zile ambazo tarehe za mwisho wa matumizi zimehaririwa," alisema. Pia alsiema uwapo wa bidhaa zilizoisha muda wa matumizi na zile zenye viambato sumu zinaathiri uchumi wa nchi pamoja na afya za watumiaji.

Alisema bidhaa za vyakula zilizoisha muda wa matumizi na zile ambazo tarehe za mwisho wa matumizi zimehaririwa, zinaathiri upatikanaji wa virutubisho vinavyotegemewa na zinaweza kusababisha magonjwa ya muda mfupi na mrefu ikiwamo saratani.

"Kwa upande wa vipodozi hasa vile vyenye viambato sumu, athari zake ni za muda mfupi ikiwamo kuathiri ngozi, macho, mfumo wa uzazi kwa kinamama, ukuaji kwa watoto na magonjwa ya saratani hasa ngozi," alisema.

Hata hivyo, alisema ukaguzi unaofanywa kwa ajili ya kutambua bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu ni endelevu kwa mikoa yote na kutoa wito kwa wafanyabiashara kukagua bidhaa zao mara kwa mara kujiridhisha na ubora wake.

"Kutunza bidhaa hizo kwa mujibu wa taratibu za wazalishaji, kuepuka kuuza bidhaa za vipodozi zenye viambato sumu na kuacha mara moja kuhariri taarifa za mwisho wa matumizi," alisema.

Alionya kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wafanyabiashara wasio waaminifu kwa mujibu wa sheria na kanuni zake.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu akizungumza katika kikao kazi kati ya wizara na wadau, kwa ajili ya kukusanya maoni ya marekebisho ya Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009, jijini Dodoma juzi. **PICHA: WAMJW**

# DC ataka trafiki kasi utoaji elimu ya usalama barabarani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, ameagiza Jeshi la Polisi kupitia kikosi cha usalama barabarani kuongeza bidii katika utoaji wa elimu ili kukomesha vifo vya watoto vitokanavyo na ajali za barabarani. Shekimweri aliyasema hayo juzi alipokuwa akitoa zawadi kwa wanafunzi wa shule za msingi jijini hapa zilizoshinda shindano la michoro ya usalama barabarani kwa mwaka 2020/21, lililoandaliwa na Puma Energy Tanzania Ltd kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la AMEND.

Alisema takwimu za watu wanaopata ajali za barabarani bado ni kubwa na kwamba kuna haja ya kuongeza elimu ili kupunguza au kuondoa kabisa vifo vya watoto, wazee na wenye ulemavu.

"Nawaagiza Jeshi la Polisi kikosi cha usalama barabarani jijini Dodoma kuongeza mafunzo kwa wanafunzi ambao wamekua wakisimama barabarani kuzuia magari ili wanafunzi kuvuka sambamba na kuwapatia vifaa," alisema.

"Tutaendelea kusimamia sheria ya usalama barabarani. Nitoe rai kwa Jeshi la Polisi kuwa wakali kwa wanaovunja sheria za barabarani, haiwezekani mtu anatembea mwendokasi sehemu ambayo kibao kinamwonyesha kutembea mwendo mdogo. Polisi mkimkamata mtu mara nyingi zaidi basi ikiwezekana anyang'anywe leseni yake," alisema Shekimweri na kuongeza kuwa ameguswa na mafunzo hayo kwa kuwa yatasaidia kuokoa maisha.

"Nimekumbuka mbali sana kwani kuna mdogo wangu alipata changamoto kutokana na ajali, ni tukio ambalo sitalisahau katika maisha yangu. Niwapongeze kwa hatua hii ya kutoa mafunzo usalama barabarani," alisema.

Mwakilishi wa Kampuni ya Puma Energy Tanzania, Mwanasheria Goodluck Shirima, alisema kampuni yao inawaowajibu kuhakikisha wanatoa elimu ya usalama barabarani kwa kuwa wanahusika na uuzaji wa mafuta.

"Lazima tusimamie usalama wa watu wote na hasa wanafunzi. Kuna msemo unaosema mtoto mkunje angali mbichi, hivyo lazima elimu itolewe kwa wanafunzi kwa ajili ya usalama wao. Tunahitaji kuwa na kizazi cha sasa na baadaye kilicho salama. Jiji la Dodoma linakua kwa kasi kubwa, magari yameongeza, hivyo Puma tutaendelea kushirikiana na serikali na wadau wengine katika kuendelea kutoa mafunzo ya usalama barabarani," alisema.

Naye Mkaguzi Msaidizi wa Polisi ambaye amemwakilisha Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Leonce Kaimukirwa, alisema wamefurahishwa na mafunzo ambayo yamekuwa yakitolewa na AMEND kwa kushirikina na Puma Energy Tanzania na kwamba jeshi hilo litaendelea kutoa mafunzo ya usalama barabarani.

Meneja Mkuu wa AMEND Tanzania, Simon Kalolo, ambaye amemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, alisema wamekuwa wakitekeleza miradi mingi katika zaidi ya nchi 10 barani Afrika, Tanzania ikiwamo.

"Mradi mmojawapo ambao tunautekeleza ni wa elimu ya usalama barabarani. Ajali bado ni changamoto (tatizo). Zaidi ya watu 350,000 duniani wanapoteza maisha na wengine zaidi ya milioni tatu wanabakiwa na ulemavu, hivyo jitihada zinahitajika. Mbali ya elimu pia kumefanyika mashindano ya michoro ya usalama barabarani," alisema.





# Mwinyi aahidi ulinzi viwanda vya ndani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Serikali itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kufanyia biashara kwa kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani usio halali kutoka nje. Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika hafla ya ufunguzi wa viwanda vidogo vilivyoko maeneo huru, Amani, mjini Zanzibar.

Katika hafla hiyo, Rais alizindua kiwanda cha vifaa vya umeme, cha kuchambua korosho, cha kutengeneza boti na cha ufungaji wa korosho, sambamba na kufungua kiwanda cha vipodozi, kilichoko Maruhubi.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuanzia sasa mkazo utawekwa katika ununuzi wa bidhaa za ndani, sambamba na kuhakikisha bidhaa zote kutoka nje zinalipiwa ushuru kikamilifu.

Alisema kuna umuhimu wa kulinda viwanda vya ndani, hivyo akaitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Shirika la Viwango (ZBS) na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kuhakikisha inalinda viwanda vya ndani kwa wafanyabiashara kulipa kodi kikamilifu.

Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kuwapongeza wawekezaji wa ndani na kuwataka wawekezaji wengi zaidi kujitokeza ili kujenga uchumi wa taifa.

Aliwapongeza wafanyabiashara kwa kazi nzuri ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha biashara, kwa kuongeza thamani ya bidhaa mbalimbali kutoka Tanzania Bara, zikiwamo korosho.

Pia alizitaka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda pamoja na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA) kuandaa eneo la viwanda vikubwa ili ifikapo mwaka 2022 lifunguliwe, kwa lengo la kupanua wigo wa uzalishaji wa ajira.

Dk. Mwinyi aliipongeza ZIPA kwa kutekeleza agizo la kulibadili eneo la viwanda vidogo la Amani kuwa eneo la uwekezaji badala ya maghala ya kuhifadhia bidhaa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Shariff Ali Sharrif, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja tangu Rais Dk. Mwinyi aingie madarakani, mamlaka hiyo imesajili miradi 97 yenye thamani ya Dola milioni 788 na kutoa ajira ya watu wasiopungua 7,000.

Alisema hayo ni mafanikio makubwa kwa kuzingatia kuwa katika kipindi kama hicho cha mwaka uliopita, Mamlaka ilisajili jumla ya miradi 30 yenye thamani ya Dola Milioni 78 na kutengeneza ajira zipatazo 1,213.

"Hii ni sawa na kusema katika kipindi hiki cha mwaka mmoja cha uongozi wa Dk. Mwinyi, kumekuwa na ongezeko la miradi kwa asilimia 323," alisema.

Ufunguzi wa viwanda hivyo ni miongoni mwa maadhimisho ya mwaka mmoja tangu Rais Dk. Mwinyi kuapishwa kuwa Rais wa Zanzibar, hatua ambayo inaonyesha mafanikio makubwa katika uongozi wake.



Sehemu ya viongozi mbalimbali wakifuatilia kwa makini hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Kumbukizi ya Maisha ya Maalim Seif Sharif Hamad, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Katibu mkuu abainisha wigo wa serikali katika ajira kwa vijana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Sanaa na Michezo, Fatma Hamad Rajab, amesema Serikali ya Zanzibar na ya Tanzania zimekuwa na wigo mpana katika kuwaunga mkono vijana katika kujiajiri.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya sekta bunifu kwa vijana katika ukumbi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mazizini mjini Zanzibar.

Fatma alisema sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kuchangia maendeleo ya vijana hasa kuwajengea uwezo wa kujiamini ili kujikimu na maisha katika nafasi za ajira.

Alisema hivi sasa vijana wengi wameondokana na mawazo mgando ya kuwa lazima kufanya kazi serikali na si kujiari.

Iwapo wabunifu watatumia vyema uwezo walionao katika kubuni fani zao, alisema inawezekana ikawa nafasi ya kujiajiri na kuwaajiri wenzao.

Naibu katibu mkuu huyo alisema Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) bado ina haja ya kuzishauri serikali zote mbili katika kufanikisha maendeleo ya wabunifu hasa wasanii wa ndani.

Alisema katika kuendelea kufikia maendeleo ya wabunifu lazima TPSF iweke mwavuli mmoja kwa Tanzania nzima ili kuleta maendeleo.

Akitoa mada katika mafunzo hayo, mshauri elekezi kutoka TPSF, Nicholas Hoseal Mbwangi, alisema katika kuwajali wabunifu lazima kuwe na mfumo ambao utakuwa mzuri kiupande wao.

Mbwangi alisema licha ya Tanzania Bara kuwa na mfumo wezeshi kwa wabunifu, bado kuna changamoto nyingi katika kufikia malengo ya mfumo huo.

Alisema kwa upande wa Zanzibar, mfumo wa kuwawezesha wabunifu bado haujaanzishwa, hivyo kuna haja ya kuanzishwa kwa maendeleo ya wabunifu katika kufanya kazi zao na kujipatia riziki. Sambamba na hilo, alisema hivi sasa vijana wengi hawana haja ya kuwa na mtazamo wa kusubiri ajira kutoka ndani ya serikali na kuanza kutupa muda wao bure bali jambo la msingi ni kuwekewa mfumo mzuri wa kuwawezesha wabunifu.

Alisema katika kufikia malengo la kupata mfumo ambao utakuwa na tija kwa vijana wa Tanzania lazima elimu ya ubunifu itolewe shuleni .

Mratibu wa TPSF, Jane Gonsalves, alisema wakati umefika kwa vijana wasiwe na zana ya kutafuta elimu kubwa ya juu wakati wanauwezo wa kufanya ubunifu na kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao .

Alisema kuna vijana wengi wa Kitanzania wamekuwa wakihangaika na vyeti kwa kusubiri ajira kutoka serikalini wakati wanao uwezo wa kubuni kazi ya kufanya.

# JK ahimiza umuhimu ukarabati wa UDSM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, amesema kuharakishwa kwa ujenzi wa chuo hicho Zanzibar ambacho hivi karibuni kiliteketea kwa moto, kutaijengea sifa na haiba nzuri Zanzibar.

Amesema hali hiyo inatokana na chuo hicho kimo ndani ya hifadhi ya Mji Mkongwe ambao ndio kitovu cha utalii.

Akizungumza juzi mjini hapa wakati wa ziara ya kukagua athari zilizojitokeza kutokana na moto huo, Kikwete aliitaka serikali ya Zanzibar kuharakisha taratibu za ukarabati wa ujenzi wa chuo hicho na haipendezi kuona ujenzi huo unachukua muda mrefu.

Dk. Kikwete ambaye pia ni Rais Mstaafu wa Tanzania, alisema uwezo wa kujenga jengo hilo wanao na wataalamu wote wakiwamo wahandisi wanaofundisha katika chuo hicho.

Pia alisema hivi sasa kazi itakayoanza ni kuja kwa wataalamu kwa ajili ya kufanya tathmini ya ujenzi huo na kuona jengo hilo linajengwa upya ikiwamo maabara kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wanaendelea na masomo.

Aliwapa pole watendaji wa chuo hicho kwa yote yaliyotokea huku akisema ajali haina kinga lakini maisha lazima yaendelee kwa kuhakikisha wanafunzi wanaendelea kupata mafunzo ya nadharia na vitendo.

Kikwete alimtaka mkandarasi aliyopewa ujenzi wa maabara katika eneo lingine la chuo hicho kilichoko Buyu nje ya Mji wa Zanzibar, kuhakikisha anamaliza kazi yake kwa wakati na ujenzi wake unakuwa katika ubora unaotakiwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka, alisema ukarabati unaofanyika Mji Mkongwe ni lazima ufuate masharti ya mji huo, hivyo watahakikisha wanashirikiana na wataalamu wa chuo na wale wa Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ili masharti yaliyowekwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) yanafuatwa katika ujenzi huo.

**Amesema hali hiyo inatokana na chuo hicho kimo ndani ya hifadhi ya Mji Mkongwe ambao ndio kitovu cha utalii.**



# Mary G, hivi ulimpataje Barnaba?

MSANII anayekuja juu kwenye muziki wa kizazi kipya kwa sasa, Mary G, ameeleza kuwa haikuwa kazi rahisi kumpata msanii Barnaba kwa ajili ya kumshirikisha kwenye ngoma yake mpya 'I Feel You'.

Ngoma hiyo kwa sasa ina siku tatu tu tangu itoke, lakini imeonekana kubamba, msanii huyo akiendeleza kile ambacho alikifanya kwenye ngoma zake zingine za 'Take Over' na 'Promise'.

'Kwanza nilikuwa na hofu. Unajua Barnaba ni msanii mkubwa, lakini mpaka yeye ameweka mashairi yake na amekubali kuimba, ina maana alikubali kazi yangu, asingeweza kukubali kujishusha," anasema msanii huyo, anayekiri kumhusudu mno Maua Sama.

"Kila kitu kina ugumu. Niliandika nyimbo, jinsi maneno yake na sauti yake, nilifikiria haraka nikaona Barnaba anafaa kuimba," alisema.

Anasema kuwa hakutegemea mapokezi mazuri ya nyimbo yake, kwani imekuwa ina mashabiki wengi, licha ya kuwa ni muda mfupi tu tangu itoke.

"Kila nyimbo inapokelewa tofauti, kila ninapoimba na kutoa nyimbo ninaonekana ninazidi kukua na mashabiki kuendelea kupenda nyimbo zangu."

Msanii huyo ambaye baadhi ya mashabiki wa muziki wamemtabiria kuwa huenda hivi karibuni anaweza kuwa kwenye anga moja na kina Nandy, Rubby, Zuchu, Maua Sama na wengine, amesema kuwa angetamani kufanya kazi na wasanii hao, lakini si kwa sasa.

"Sina muda mrefu kwenye muziki, kwanza napambana, naangalia kwanza upande wangu, halafu hapo baadaye naweza sasa nikataka kumshirikisha msanii yoyote wa kike," alisema na kuonyesha kabisa kuwa kwanza na yeye anahitaji awe na jina na si kubebwa zaidi na wasanii nyota wa kike.

Mary G, anabainisha kuwa ngoma zote alizotoa ni kwamba mashairi anayaandika mwenyewe na amekuwa akizingatia zaidi staili ya uimbaji 'melody' kuliko mashairi ili kuifanya nyimbo zake ipendwe.

"Unaweza ukawa na mashairi mazuri sana, lakini 'melody' ikiwa mbaya, wimbo hautopendwa na mashabiki wengi. Ila unaweza kuwa na 'melody' nzuri, hata kama mashairi hayakuwa mazuri, lakini mashabiki wataupenda, kwa hiyo mimi kwanza kabisa nazingatia 'melody'." Anasema Mary G.

BASI SAWA

## Fobby acha waganga, piga kazi tu



NILIWAHI kwenda kwa mganga. Kuna mtu aliniambia oya, kuna shoo fulani iliandaliwa sehemu, jamaa akanambia muziki wako mkubwa sana, wewe jina lako wamefukia. Ngoma zako muziki wako mkubwa sana, wewe wameroga jina lako, lakini ngoma zako wanazijua sana, kila mtu anazo kwenye simu. kila ngoma yangu nashuti video, lakini nikitokea hakuna mtu ananijua. Video zinaonekana, lakini nikitokea hapa watu hawanijui. Basi kuna jamaa wakanipeleka. Lakini huwezi kuamini, hakuna kitu chochote kile. Kwanza ndiyo kwanza tulipata ugumu kwenye kurekodi. Vitu vyenyewe zikuvitumia. Mimi nasali sana, halafu nianze kuoga dawa. Huku Mungu huku mambo haya. Halafu sikutoa pesa. Nilipewa na huyo aliyenipeleka na kutaka nikapige kwenye shoo yake.

Siyo mwonekano wangu. Mimi siyo mtu wa matukio, hunikuti kwenye matukio yoyote. Mimi nimejiwekea 'Kutamu' Ngoma yangu imeshika namba moja Zambia na inatamba Nigeria

'Kutamu', 'Ode', 'Niokoe', 'Bwana Mkubwa', 'Kitanda' na zingine nyingi

## Best Naso yuko fiti kalikiti

MSANII wa nyimbo kali za masikitiko, Best Naso, amebainisha kuwa bibi yake alizirai mara tatu, baada ya kusikia uvumi wa kwamba amejinyonga.

Mwezi Machi, mwaka huu, mtandao mmoja huko nchini Kenya ulizusha taarifa za kifo cha msanii hiyo kuwa amefariki kwa kujinyonga.

Best ameeleza madhara ya habari ile kuwa bibi yake kijijini alizirai mara tatu na baada ya hapo ilibidi ampigie simu ili athibitishe na kukuta si kweli.

"Mimi mwenyewe nilikutana na hiyo taarifa kwenye blogu moja ya Kenya. Nilishtuka, lakini nikasema basi, nisiposemwa mimi nani mwingine atasemwa. Lakini bibi na dada yangu walishtushwa sana taarifa ile ya uongo," alisema.

Best ambaye kwa sasa ameachia 'albamu' inayokwenda kwa jina la 'Gift of Life', anasema kuwa tayari ameachia singo ya video ya 'Walikuwepo', ambayo ni moja kati ya ngoma zilizopo kwenye albamu hiyo kali yenye pini 32 za maana.



Akaongeza kuwa kwa sasa anaendelea kupiga shoo kama kawaida, na hajafulia kama baadhi ya watu wanavyodai na ndiyo maana ametoa albamu yenye ngoma kibao, tena kali.



## Nay wenyewe wakikusikia weweee

NAY wa Mitego katoa mpya. Siyo ngoma mpya, hapana. Anasema eti yeye kuoa bado kabisa, bado yupo yupo sana. Hadi hivi sasa anasema akiwatazama washkaji zake ambao wameoa, hawamshawishi yeye kufanya hivyo.

"Kwangu mimi kuoa siyo kitu kikubwa sana. Mimi kuoa siyo kila kitu kwenye maisha. Nimeona watu wanaoa, lakini baada ya miezi mitatu wanaachana. Na hata waliooa hawanifanyi kuwa na hamu ya kuoa. Mtu anaoa leo, baada ya siku tatu au nne tunagombania nao demu," Nay alitoa siri.

Akaweza wazi kuwa watu wasitegemee kumuona rais wa kitaa akaingia kwenye ndoa mapema kwa sababu anaona atamuumiza mwanamke atakayemuoa.

"Mimi sitaki kumuumiza mtoto wa watu. Bado nina mambo mengi. Ila nina mtu moja nipo naye, ananipenda na nampenda. Tunaheshimiana, maisha yanaenda. Siku nikiona muda sahihi wa kuona nitaona. Ina maana hapo sasa nitaamua kuacha kila kitu," Nay huyo anasema hivyo.



## Marafiki watatu kwa mpigo

KIKUNDI cha nyimbo za Injili cha 'The Friends of Jesus' cha Kanisa la Waadventsita Wasabato Mbezi Luis Dar es Salaam, kimezindua albamu tatu kwa mpigo za kutambulisha uwepo wa kikundi hicho.

Majina ya albamu hizo ni 'Shangwe, Ni Mwema na Jina la Yesu', ambazo zilizinduliwa mwishoni mwa wiki iliyopota na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya Tanzania (TUGHE), Hery Mkunda.

Mkunda aliyekuwa mgeni rasmi, amewataka waimbaji wa kikundi hicho kuendelea kufanya kazi ya Mungu kupitia uimbaji ili ujumbe walionao uweze kupenya kwa watu wengi zaidi ili waokoke.

"Niwapongeze The Friends of Jesus kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huu na pia ninaomba muendelee kuwa na umoja huu ili mfikishe habari njema ya Mungu kwa watu wengi zaidi," amesema Mkunda.

Naye kiongozi wa kikundi hicho, Veronica Balula amesema, kilianzishwa mwaka 2012, lakini tangu wakati huo kilikuwa hakijazindua albamu kutokana na sababu mbalimbali ambazo ziko juu ya uwezo wa kikundi hicho.

## LUGHA ZA KIASILI TAMU KWENYE MUZIKI

**Na Adam Fungamwango**

HIVI wasanii wa bongo fleva mnakwamba wapi? Hivi sasa huwezi kusikia nyimbo zilizoimbwa kwa lugha za makabila ya Tanzania. Wasanii wa muziki wa kisasa wa bongo fleva na hata dansi kwa sasa wamekuwa wakiimba kiswahili tu. Bongo fleva wao wakibadilisha, basi wataimba kingereza. Baadhi wanakwenda mbali zaidi hadi Kiganda wanaimba. Ni mara chache sana kusikia nyimbo za lugha za makabila ya Tanzania. Nchi hii ina makabila zaidi ya 120, ingekuwa vizuri zaidi wasanii wetu baadhi ya singo zao wangekuwa wanaimba kwa kilugha.

Labda wanaangaliza soko zaidi. Hata hivyo nina uhakika, msanii akitunga wimbo wa kabila lolote la Tanzania, ikiwa kwenye redio, televisheni na hata mitandao ya kijamii, itapata wasilikizaji na waangaliaji wengi. Wapenzi wa muziki siku zote hupenda kusikiliza vitu tofauti na walivyozoea.

Mfano, mwanamuziki kuimba nyimbo za kilugha ni Saida Kalori. Ushahidi tunao kuwa wimbo wake wa 'Maria Salome' ulitingisha Tanzania, hata nje ya nchi.

Hapa nchini, wanamuziki mbalimbali miaka ya nyuma, walitunga na kuimba nyimbo za makabila mbalimbali, ambazo zilivuma na kuwafanya kuwa maarufu zaidi na zaidi. Leo tuzitazame nyimbo zilizoimbwa kwa lugha za makabila ya Kitanzania na hata zikiimbwa zinapendeza masikioni.

**KILA MUNU AVE NA KWAO- TONGOLANGA**

Huu ni wimbo maarufu zaidi wa kilugha. Lugha iliyotumika ni Kimakonde, ukiwa na maana kila mtu ana kwao. Mtunzi, marehemu Harila Tongolanga, alikuwa akiwakumbusha Watanzania kuwa kila mtu ana kwao alikozaliwa na asiache kukumbuka sehemu yao aya asili alikozaliwa.

**AKULA MWEMBESONGO-MBARAKA**

Mbaraka Mwinshehe Mwaruka alikuwa na nyimbo nyingi sana za kilugha na kuziimba kwa Kiluguru.

Nimeichagua 'Akula Mwembesongo', wimbo wa Kiluguru alisimulia kisa cha kukutana na msichana mmoja aliyemwambia kuwa hana mwanaume, akampeleka hadi kwake, lakini wakati wako ndani mumewe alipiga hodi, ikabidi akimbie. Akamuachia 'msala' mwanamke.

**MWAIPUNGU-OSS**

Orchestra Safari Sound, ikiwa kwenye mtindo wa 'Dukuduku', ikiwa na wanamuziki wengi Wakongomani, lakini walitunga wimbo wa Kinyakyusa uitwao 'Mwaipungu'. Maudhui ya wimbo huo ni jamaa anamuasa mpenzi wake asisikilize maneno ya watu, kwa sababu lengo lao ni kutaka kuwatenganisha. Anamwambia waache waseme, wao waendeleze penzi lao.

**SHAKAZA-EDDY SHEGGY**

Nyimbo za 'Shakaza' zipo namba moja hadi tatu. Zote zimetungwa na mtu mmoja, Eddy Sheggy. Mbili ni za Washirika Tanzania Stars, na moja ni ya Bima Lee. Zote zinazungumzia zimeimbwa kwa lugha ya Kisambaa. Zote zina kisa kinachofanana cha mama mmoja aliyetelekezwa na mumewe, akaenda mjini kufanya starehe zake, akimuacha na watoto na kuishi maisha ya shida.

**NALILA MASUMANDA-HAMZA KALALA**

Hamza Kalala ni mmoja kati ya wanamuziki wanaopenda sana kutunga nyimbo za lugha za makabila ya Tanzania 'Nalila Masumanda' aliutunga akiwa na bendi ya Washirika Tanzania Stars, maarufu kama 'Watunjatanjata'. Lugha iliyotumika ni Kisukuma. Jamaa asikitika kutomuona mpenzi wake ambaye yuko mbali na yeye. Ng'ombe aliokuwa akitegemea kuuza ili kupata nauli ya kwenda kwa mpenzi wake.



## Chanzo ni Mama:Mke huletewi, unatafuta mwenyewe

**Na Adam Fungamwango**

KWA zama za sasa hivi mke anatafutwa, na si kuletewa kama ilivyokuwa zamani. Ni kweli, wazazi wanaweza kuwa na nia nzuri, lakini hali inapokwenda ndivyo sivyo, lawama inaangukia kwao. Ndiyo maana hata wazazi wa sasa hivi hawataki kuwatafutia vijana wao wake. Wanaogopa lawama. Wanataka kijana watafute mwenyewe. Ili yakimkuta, basi asiwe na wa kumlaumu.

Leo tunaiangalia filamu ya 'Chanzo ni Mama'. Inamhusu mama mmoja aliyetaka kulazimisha kijana wake amuoe binti wa shoga yake na siyo yule aliyempenda. matokeo yake yakawa ni maafa tu.

Filamu imechezwa na Azela Chewa, Jumanne Jackson, Anna Hamisi, Mwanahawa Hassan, Rehema Hamisi, Moshi Jumanne na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha msichana mrembo Shakira akiwa anatoka mjini amemaliza masomo yake.

Anakutana na kijana Sadam ambaye anamuonyesha njia, kwani alitoka zamani na hakuwa anajua njia vizuri.



Kuonana kwa mara ya kwanza, kunawafanya vijana hao kupendana. Sadam anatokea kumpenda Shakira, na Shakira hivyo hivyo.

Mama Sadam ana shoga yake, ambaye ni mama Salma. Kwenye vikao vyao wanapanga watoto wao waoane, Wakat Salma anakubali kuolewa na Sadam, lakini kijana huyo hataki. Mama yake anashangaa. Upelelezi ukafanywa. Ikaonekana kuwa Sadam anamhusudu Shakira na si Salma. Wazazi wanaapa kumkomesha.

Shakira anafanya kosa la kiufundi. Anakwenda kwa mpenzi wake Sadam, anamkuta mama yake, anaomba maji. Mama huyo sijui anaweza nini humo. Baada ya kunywa, Shakira anageuka kuwa kichaa. Lengo kijana wake amuoe Salma na si hiyo. Sadam sasa hawezi tena kuoa kichaa. Na hakujua kama ni mama yake amefanya hivyo. Anakubali kumuoa Salma. Ndoa ya hao wawili inakuwa na misukosuko. Salma hakuwa mwaminifu. Alikuwa na mpenzi wake mwingine anaitwa Mrisho. Siri inafichuka. Sadam anakuja kufahamu hilo. Anamfuata Mrisho na kumwambia aachane na mkewe, la sivyo atakiona. Hiyo inamshtua mno Mrisho na anachofanya ni kumvizia shambani na kumnyonga Sadam.



# Jay Z acha kuwarusha roho watu

RAPA kutoka Marekani, Jay Z, amefunga ukurasa wake wa Instagram ikiwa ni saa 24 tu baada ya kujiunga na mtandao huo.

Hatua hiyo imeleta mshtuko kwa mashabiki wake ambao walivamia ukurasa wake wa Instagram kwa shangwe kuona staa huyo kujiunga nao kwenye mtandao huo.

Wakati anafunga tayari alikuwa amekusanya zaidi ya wafuasi milioni 2.3. Pale alipofungua mnamo Jumatano, Novemba 3, mwaka huu.



## Kim aopoa Serengeti Boy

STAA wa kipindi cha maisha wa Marekani, Kim Kardashian, anahusishwa kutoka kimapenzi na Pete Davidson'.

Kulingana na mtandao wa PageSix, Davidson aliwasili jijini New York katika mgahawa wa Posh na dakika chache Kim alitokea na kwenda faragha.

Kim yupo katika mchakato wa kuomba talaka kwa aliyekuwa mume wake Kanye West ambao wamepata watoto wanna.

Pete ambaye ana umri wa miaka 27 walikula chakula pamoja kwenye hoteli hiyo na kisha kila mmoja aliondoka kivyake.

## Will Smith mkemee shetani

MUIGIZAJI kutoka Marekani, Will Smith, ameweka wazi jinsi alivyowahi kufikiria kumuua babake.

Rapa huyo mwenye vipaji vingi amekuwa akifichua mengi kuhusu maisha yake, familia, safari ya kupunguza uzito katika kitabu chake.

"Baba yangu alikuwa mjeuri, lakini pia alikuwa kwenye kila mchezo, kucheza na kukariri. Alikuwa mlevi, lakini alikuwapo katika kila onyesho la kwanza la kila filamu zangu," amesema





## Zapp kweli wewe Mjerumani?

SIO mzaha, bali ni kweli imetokea! Kwani prodyuza maarufu wa Ghana Zapp, amesema yeye ni Mjerumani lakini amejikuta mwili wake ukitupwa Ghana kimakosa.

Zapp amesema hayo wakati akishiriki katika mazungumzo kuhusu hadithi ya mtu mmoja Muingereza ambaye alitaka kupambana na ubaguzi kwa kuamua kujibadilisha sura kwa njia ya upasuaji na kuwa Mkorea.

"Najihisi Mjerumani na mwili wangu umetupwa Ghana," Feel I'm a German trapped in a Ghanaian body..." Zapp Mallet amesema kupitia Twitter.

## Cardi B hongera kumiliki mjengo

HATIMAYE rapa mwenye vituko vingi Marekani, Cardi B, amenunua jumba la kifahari katika jiji la New York.

Kupitia akaunti take ya Instagram, Cardi B, aliweka picha ya nyunba hiyo na kuandika jinsi anavyoona ufahari kumiliki mjengo huo akiwa na nguvu zake.

"Siku hizi sitaishi sehemu moja, kila mahali ninapofanya kazi nahakikisha ninakuwa na nyumba, najivunia kuwa na nyumba katika jiji hili la New York," ameandika.



MAKALA

# TaMCare na tiba migogoro ya ndoa

## ●Yaibua kliniki ya ndoa na uhusiano wa ustawi majumbani



Ongezeko la migogoro ya ndoa limesababisha watoto kukosa malezi ya wazazi pamoja na kukosekana ustawi wa jamii na taifa kwa jumla. **PICHA; MAKTABA.**

**Na Epson Luhwago**

"MIGOGORO ya ndoa imekuwa mingi na inaongezeka kila siku. Hii imesababisha ndoa kuvunjika tena nyingi zikiwa changa kabisa. Kama jitihada za makusudi hazitachukuliwa kuna hatari kubwa katika jamii na taifa. Ni vyema tukapata tiba ya ndoa kwa maendeleo ya familia, jamii na taifa."

Haya ni maneno ya Mchungaji Edson Mgeni wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani katika moja ya mahubiri yake miaka ya 2010, wakati huo akiwa Mchungaji Kiongozi Usharika wa Hananasif.

Kiongozi huyo wa kiroho alikwenda mbali zaidi kwa kusema: "Pamoja na ndoa nyingi kuvunjika, wako ambao wamekubali kufa na tai shingoni, kwa maana ya kuvumilia tu. Watu hawa ukiwaona nje wanaonekana wenye furaha lakini ndani kunawaka moto. Wako waliogawana vyumba na wengine wanalala mzungu wa nne."

Huo ndio uhalisia uliopo katika ndoa. Migogoro ndani ya ndoa na uhusiano imekuwa ikiongezeka siku hadi siku na mbaya zaidi baadhi ya ndoa zinavunjika muda mfupi baada ya kufungwa.

Mbali na migogoro ya ndoa na uhusiano ambayo imeathiri ustawi wa familia na taifa, pia kumekuwa na ongezeko la talaka katika mahakama nchini, Dar es Salaam ikiwa kinara, kama Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alivyobainisha hivi karibuni jijini Dodoma.

Mwaka 2018, kwa mfano, taarifa ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) inaonyesha kuwa talaka 3,814 zilisajiliwa kutokana na migogoro ya ndoa.

Hiyo pia inathibitishwa na mtaalamu mbobezi wa masuala ya ndoa na familia, Mchungaji Dk. Enock Mlyuka, ambaye anasema kwa uzoefu wake wa miaka 28 akiwa mchungaji, amepokea na kushughulikia mashauri mengi yanayohusu ndoa na uhusiano huku akiweka wazi kuwa hata viongozi wengine wa dini, wakiwamo mashehe na wachungaji wamekuwa wakikutana na hali kama hiyo.

"Kadri siku na muda unavyoongezeka, mashauri kuhusu migogoro ya ndoa yanaongezeka kwa viongozi wa dini. Mashauri mengine yako kwa watendaji, vitongoji, ustawi wa jamii na madawati ya jinsia.

"Hata masuala ya talaka yanaongezeka. Yanayojulikana ni yale yanayofikishwa katika vyombo vya sheria lakini wengine wanaamua kuachana au kutengana kienyeji tu," anasema.

Mchungaji Mlyuka, ambaye pia ni mwanataaluma na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care (TaMCare) Foundation, inayojihusisha na masuala ya ndoa, familia na malezi ya watoto, anasema taasisi yake imekuwa ikipokea na kushughulikia mashauri yanayohusu ndoa, ambayo ni taasisi kongwe duniani tangu kuumbwa kwa ulimwengu.

**"Pamoja na ndoa nyingi kuvunjika, wako ambao wamekubali kufa na tai shingoni, kwa maana ya kuvumilia tu. Watu hawa ukiwaona nje wanaonekana wenye furaha lakini ndani kunawaka moto. Wapo waliogawana vyumba na wengine wanalala mzungu wa nne."**

Chanzo cha migogoro hiyo ambayo imesababisha ndoa nyingi kuvunjika, kwa mujibu wa Dk. Mlyuka, ni ukatili, kukosekana kwa uaminifu baina ya wanandoa, chimbuko (asili ya miongoni mwa wanandoa), kutokushirikishana masuala yanayowahusu (ubinafsi) na hali ngumu ya maisha.

**KLINIKI YA NDOA**

Kutokana na ongezeko la migogoro ya ndoa na uhusiano, TaMCare Foundation imebuni programu maalum ijulikanayo kama 'Kiliniki ya Ndoa na Uhusiano' ambayo itazinduliwa baadaye mwezi huu, mkoani Dar es Salaam.

"Baada ya kugundua ongezeko la tatizo hili na kusababisha athari kubwa kwa ustawi wa ndoa, jamii na taifa, tumebuni progamu hii ikiwa sehemu ya kutibu chanzo cha tatizo," anasema Dk. Mlyuka huku akibainisha kuwa malengo ya kiliniki hiyo ni kujenga misingi imara ya ndoa, familia na malezi; kuwasaidia vijana kujitambua; na kusaidia afya na uhusiano.

Anasema watu wengi wamekuwa wanaingia katika ndoa na uhusiano wakiwa hawana msingi imara, ikiwamo kukosa ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi ya ndoa na wengine wanarithi au kuambukizwa tabia kuwa suala la kuoa ni sehemu ya maisha.

"Jambo la msingi katika kliniki hii ni kuwezesha vijana wajue misingi, kanuni, maadili, sera na taratibu. Vijana wajue haya kabla ya kuoa au kuolewa. Pia wazazi wafahamu umuhimu wa malezi bora na kuzaa watoto bora. Tunahitaji jamii bora ya wazazi bora," anasema.

Kiliniki hiyo, anasema ina lengo la kuwasaidia vijana kujitambua. Anasema vijana wengi hawajitambui kutokana na makuzi na malezi waliyopitia, hivyo ni lazima wafahamu kusudi la maisha yao pamoja na kujua kwamba ujana ni kipindi cha mpito kwa hiyo wanatakiwa kuandaa kesho yao sasa.

Makuzi na malezi wanayopitia vijana, Dk. Mlyuka anasema yamesababisha baadhi yao kutokutambua umuhimu wa muda, kufanya kazi kwa bidii na wajibu wao katika ndoa na uhusiano.

"Mfano mtu ni mfanyakazi lakini badala ya kufanya kazi, muda mwingi anautumia kucheza na simu tena kwa mambo yasiyofaa. Kijana akiingia katika ndoa hawajibiki kwa mwenza wake na kwa watoto. Wengine hawajui hata kupika. Hiyo yote ni kutokujitambua.

"Hata wanapokuwa masomoni, vijana wanafanya mambo ya anasa tofauti na yaliyowapeleka. Pia wanakosa nidhamu ya muda na matokeo yake ni majuto. Yote hayo yanatokana na kutokujitambua. Kliniki hii inakusudia kuwasaidia vijana kujitambua na kuwa wanandoa imara na hazina kwa taifa," anasema.

**AFYA NA UHUSIANO**

Migogoro katika ndoa imesababisha athari kubwa za kiafya ikiwamo afya ya akili, msongo wa mawazo, shinikizo la damu, kisukari, kiharusi na hata wengine kupoteza maisha kwa kujiua kwa kujinyonga au kumeza vidonge.

Kutokana na athari hizo, Dk. Mlyuka anasema kliniki hiyo inaweka mkazo katika afya na uhusiano ili kuhakikisha athari zinapungua kwa baadhi ya wanandoa kujiepusha na viashiria vinavyoweza kuathiri afya zao.

Anasema ndoa ni kitovu cha maendeleo ya familia, jamii na taifa, hivyo kunapokuwa na migogoro, athari kubwa za kiuchumi, kiroho na kijamii zinajitokeza, hivyo huathiri mfumo mzima wa maisha.

"Ndoa zinapokuwa na migogoro au kuvunjika, athari zake ni kubwa kwa watoto, wanandoa wenyewe na wazazi wa pande zote. Hata ufanisi katika mambo mbalimbali unapungua, afya zinadorora na kuathiri ustawi wa familia, jamii na taifa.

"Ni lazima tutambue kuwa bila ndoa imara hakuna taifa, jamii wala familia imara. Maendeleo ya taifa yanahitaji ndoa imara, hivyo ni lazima tutafute tiba ya migogoro ya ndoa ili kuwa na taifa imara," anasisitiza.

Ili kuhakikisha mpango huo unafanikiwa, Dk. Mlyuka anasema taasisi yake itajikita katika kutoa elimu juu ya ndoa na uhusiano; kutoa elimu kuhusu talaka na mirathi; elimu ya afya, lishe na malezi bora ya watoto, elimu ya kujitambua na maarifa ya nyumbani kwa vijana; na ushauri kuhusu ndoa na familia.


Dk Enock Mlyuka

# Uongozi shule Kadama waorodhesha silaha zake za ushindi darasa la saba

## ●Medani za darasani, mijadala, motisha ...
## ●Namna wanaokwama huvushwa, michezo

**Na Mwandishi Wetu,** CHATO

IMETIMU wiki sasa tangu kutangazwa matokeo ya mtihani wa darasa la saba nchini na joto la mjadala wake bado umezama zaidi katika jamii, hasa kuhusu mustakabali wa maendeleo ya mtoto na familia yake.

Naam! Waliovuna matokeo bora wapo, vivyo hivyo walioshindwa hawajakosekana. Mara zote ili mtu afanikiwe, wataalamu wa elimu katika nadharia yao humuangalia mwanafunzi katika sura tatu kuu; kijamii, kisaikolojia na falsafa zake.

Hicho ndicho chenye mchango mkubwa katika kumfanikisha kitaaluma mwanafunzi, akiwa ameiva pia ndani ya 'vigezo na masharti' viwili muhimu; nadharia na vitendo.

Hapo ndipo mtu akisafiri kusaka tafsiri ya mafanikio katika Shule ya Msingi Kadama, ambayo katika taarifa hiyo yenye wiki inakalia nafasi ya kwanza wilayani Chato na ya pili mkoani Geita, sura ya agalizo hilo halikosekani.

Hata hivyo, ufanikishaji wa anachokilenga kuna nadharia na vitendo. Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kadama, Ikigo Kihamba, anataja siri ya mafanikio katika maeneo kadhaa kama vile zawadi kwa wahusika, punguzo la malipo na washindi kupatiwa pesa taslimu.

Kuna anachokisisitiza kwamba, ili mwalimu awe na juhudi za kutosha yampasa kuwa na wito wa kazi yake ambayo muda wote atakuwa na nia ya kutimiza wajibu wake ipasavyo kwa kuwa karibu na wanafunzi wake.

Anautaja huo ni wito umekuwa ukiwasukuma walimu wa shule ya Kadama kubuni njia mbalimbali za kuwasaidia wale watoto wenye uelewa wa chini, ili nao waweze kwenda sawa na wenzao.

"Mojawapo ya mbinu hizo ni kuunda makundi ya mchangayiko wa watoto wenye uelewa wa chini, kati na wa juu ambao wamekuwa wakifundishana 'wao kwa wao, lakini chini ya usimamizi wa mwalimu husika," anafafanua.

Unaliunganisha na namna uongozi wa shule unatoa motisha kwa walimu na wanafunzi wanaofaulu mitihani shuleni, wakipewa zawadi kama punguzo la ada, hasa kwa wanaopata alama za ufaulu kati ya 45 na 50.

Kwa mujibu wa Kihamba, mtoto kupitia ziara za mafunzo anazopelekwa, anapata uelewa na kujifunza kwa vitendo na hata kwenda kuyaendeleza katika maisha yake, akisisitiza shule kuzipa kipaumbele.

Mwalimu huyo anataja lingine, ni namna wanakuwa wabunifu wa makundi ya kuwasaidia wenye uelewa wa chini, ili kwenda nao sawa.

"Kuna wakati ambao wamekua wakifundishana wao kwa wao, lakini chini ya usimamizi wa mwalimu husika," anaeleza Mwalimu Kihamba, anayedokeza ufaulu kushika nafasi ya juu shuleni kwake si mara ya kwanza.

Ni namna ya ufaulu ambao mzizi wake unaanzia kwa mtoto anapofanyiwa majaribio wengi, wengi wanamudu alama ya ufaulu mzuri isiopungua alama 40 kati ya 50.

Lakini, ili kujitahidi asiwe nje ya maudhui, Mwalimu Mkuu anaelekeza imani yake katika mbinu ambayo kwa kiasi kikubwa imezaa matunda, kwa walimu wanamaliza maudhui ya mwongozo wa mtaala (syllabus) mapema kabla ya mitihani.

Anasema, kwa utaratibu wao huwa wanajitahidi kufanya hivyo, kwani inawapa muda walimu na wanafunzi wao kufanya marudio na maboresho penye udhaifu.

Mwalimu huyo anasema ni utaratibu wao kila mwaka, iwe kwa mtihani ya mwisho wa mwaka au wa taifa na kwa kawaida huwa wanamaliza 'silabasi' wastani wa miezi mitatu kabla ya kipindi wanachopaswa, hivyo inawawezesha kujinoa na mtihani husika.

### NGUVU YA MOTISHA

Mwalimu Mkuu Kihamba, anataja siri nyingine ya ufaulu yenye sura tofauti, ni pamoja na uongozi wa shule kutoa motisha kwa walimu na wanafunzi, pale vijana shuleni wanapofaulu mitihani ya majaribio.

Anataja sehemu ya vigezo vya kutolewa zawadi ni kwa wanafunzi wanaobahatika kufikia ufaulu, ikiwamo wastani wa alama kati ya 45 na 50.

Mkurugenzi wa Shule, Leticia Bilali, anaunga mkono hoja hiyo kwamba motisha ni chachu kubwa katika kukuza ufaulu shuleni, akifafanua zawadi husika ni zile zinazowagusa wahusika moja kwa moja, wanafunzi na safu ya watumishi wote wakiwamo wasio walimu.

Kwa mujibu Mkurugenzi, wanafunzi wanahamasishwa kwa punguzo la ada zinazowahusu walio katika madarasa yanayofanya mitihani ya taifa, ambayo ni la nne na saba.

Ni punguzo la asilimia 20 kwa wale wanaopata alama kati ya 45 na 50 katika mitihani ya majaribio na mlengwa hunufaika na punguzo hilo kwa mwaka huo husika (la nne au saba).

Sambamba na hilo, kila anayefaulu vizuri hupewa ofa ya chakula anachokipenda, pamoja na vifaa mbalimbali vya darasani.

"Pia, wanafunzi hawa hawachangii gharama za kwenda ziara za masomo kwa vitendo, shule inawagharamia" anasema.

Upande wa watumishi, mkurugenzi anasema inawajumuisha walimu na watumishi walioko katika kada nyinginezo kama vile wapishi, walinzi na wana- mazingira.

Walimu nao hupewa motisha mbalimbali, ikiwamo pesa taslimu na mavazi kama vile suti kwa wanaume na vitenge kwa wanawake.

Mkurugenzi anaeleza kwamba, shule imekuwa ikitoa mikopo isiyo na bila riba, kuanzia Sh. millioni mbili na kumtaka mwalimu kulipa kwa awamu anazoona zinafaa.

### KUPITIA ZANA MICHEZO

Mwalimu wa Michezo shuleni hapo, Steven Kakonyo, anaeleza namna michezo inavyowaongezea wanafunzi uelewa darasani, kwani ikianzia na kuwaweka sawa afya ya mwilini na akili.

Anarejea wanachoelekeza wataalamu wa afya, shule inalenga kukuza vipaji vya watoto kupitia michezo inayofanyika mara kila mara shuleni hapo.

Mwalimu wa Michezo anakiri mabadiliko kwa namna ambavyo wamekuwa wakionyesha vipaji mbalimbali vya michezo katika riadha, kuruka kamba, kuimba na kuigiza, sambamba na kucheza mipira kama ya miguu, pete na mikono.

Rai yake ni kwa serikali kuweka mkazo na mfumo rasmi wa kukuza vipaji vya watoto katika shule zote za msingi na sekondari, iwe binafsi au ya umma.

"Kwa sababu michezo ni ajira, shule yetu imejidhatiti kuendeleza vipaji vya watoto tunavyoviibua, lakini bahati mbaya tunaachana nao pale wanapomaliza darasa la saba. Tunaomba ngazi zinazofuata zisaidie kuendeleza pale tunapoishia sisi wa shule za msingi," anashauri.

Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) Jumamosi wiki iliyopita, ilitangaza matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka huu 2021, yakionyesha wanafunzi 907,802 kati ya 1,107,460 sawa na asilimia 81.97 wamefaulu, huku mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiongoza.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk Charles Msonde, anasema katika shule 10 bora kitaifa Kanda ya Ziwa inaongoza kuwa na shule nane.

Anazitaja inayoongoza ni Graiyaki ya mkoani Mara. Pia, zimo St Peter Claver (Kagera ), Rocken Hill (Shinyanga), Kemebos (Kagera) Bishop Caesar (Kagera), St Marget (Arusha), Waja Springs (Geita), Kadama (Geita) na Chalinze Modern Islamic (Pwani).






Picha tofauti za wanafunzi wa Shule ya Msingi Kadama, iliyoko mkoani Geita, wakiwa kwenye ziara ya mafunzo katika kiwanda cha kutengeneza vinywaji baridi, jijini Mwanza. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

## ILIVYOKUWA ZAMANI, LEO & YAJAYO...

# Majina ya miji, mikoa ilivyogawanyika kwa mizizi tofauti, kila moja maana yake

**Na Adam Fungamwango**

WIKI mbili zilizopita gazeti hili lilibua simulizi ya mzizi na maana ya majina ya vitongoji vya jiji Dar es Salaam. Wasomaji wengi waliguswa na kutaka mustakabali mpana, jijini na kitaifa. Nipashe ikaridhia kuwasilisha kitaifa na kwa mapana.

Kimsingi, hakuna majina ya mikoa, wilaya, mji, vitongoji au vijijini ambayo hayana maana, au asili ya kuitwa hivyo. Kwa Tanzania, sehemu zote zina maana ambazo zimeganyika kwenye sehemu tofauti.

Majina hayo yanatokana na athari za majina ya kigeni, lugha za makabila ya asili au Kiswahili. Mtu anaweza kukuta jina fulani lilianza kuitwa na Wakoloni na Kijerumani au Kingereza, na wenyeji wakashindwa kutamka kwa ufasaha jina hilo kutokana na athari za matamshi.

Pia, iko kinyume chake kwani kuna majina yalianza kwa kuitwa na wazalendo kwa Kiswahili au lugha za makabila na wazungu wa kikoloni, wakashindwa kutamka sawasawa, ikaendelea hivyo hadi ikawa mazoea.

Majina mengine yanatokana na historia ya eneo kama vile vita, utumwa na mambo mengine yanayofanana na hayo. Zipo sehemu ambazo majina yake yametokana na watu maarufu wanaoishi maeneo hayo.

Mfano hai ni Buruguni kwa Malapa au Buguruni kwa Kimbengele. Wazee Kimbengele na Malapa, walikuwa maarufu sana maeneo ya Buguruni, Dar es Salaam wastani wa zaidi ya miaka 50 au 60 iliyopita.

Pia, kuna eneo la Msasani, Dar es Salaam, inayoelezwa mzizi wake ni kuwapo mnyapara aliyekuwa anasimamia mashamba ya katani akitokea Mtwara.

Kutokana na hilo, wenyeji wengi kutoka mkoa huo walikuwa wakimiminika kwenda kuomba kazi kwake na kwa kiasi kikubwa walikuwa hawapajui, hivyo waliuliza kwa mnyapara huyo kuliko. Walihoji kwa

lafudhi akitamka wapi kwa 'Mucha Hachani') kwa maana ya Mussa Hassan.

Ni matamshi yaliyoendelea na mazoea katika mazoea ya matamshi hayo, hata yakahamia katika lugha ya kurahisisha Msasani, baada ya kuvuka mpito wa 'Mchachani.''

Eneo jirani na Msasani, Kawe kiote katika wilaya ya Kinondoni, kulikuwapo kiwanda cha kuandaa nyama maarufu Tanganyika Packers. Hapo kulikuwa machinjio rasmi ya ng'ombe.

Ili kufika ng'ombe mahali hapo, barabara au njia maarufu uliyotumia kuwaswaga ng'ombe kutoka ikaitwa 'cow way', kwa maana yake 'njia ya ng'ombe.'



Mandhari ya Mwananyamala, jijini Dar es Salaam sasa, ambako kihistoria kulikuwa porini hata kuwapo na angalizo la wazazi 'mtoto nyamaza' kuhofia wanyama.

Ulikuwa mtihani kwa wengi kutamka msamiati huo wa kizungu. Wengi walishindwa na wakaangukia msamiati uliojichimbia sasa, Kawe, huku eneo la Kigogo lilitokana na kuwapo daraja la Kigogo cha Mnazi.

Tabata wilayani Ilala, kuna historia ya kuwapo mkazi wa jamii ya Kiarabu, aliyekuwa mnunuzi wa jumla wa korosho kwa mali kauli, akiahidi siku fulani ya malipo.

Lugha yake ya uungwana wa kubembeleza katika biashara, ndio ilizaa msamiati Tabata, kupitia kauli yake ya ahadi ya kulipa katika lafudhi ya kiarabu 'habana tabu tabata', akiwa na maana watapata pesa zao. Akajikuta anapachikwa jina la 'Mwarabu Tabata', mwishowe eneo zima umarufu wake ukabali kuwa Tabata.

Kitovu cha masoko katikati ya jiji la Dar es Salaam, eneo maarufu kitaifa na kimataifa, Kariakoo, jina lake ni zao la athari ya Waswahili kushidwa kutamka neno la Kiingereza 'carrier corps' ikiwa na maana wabeba mizigo.

Kwa wakati huo wenyewe waswahili walikuwa wakiwaita makuli, ambao nalo ni zao kutoka kiingereza 'Coolie' kwa maana ya kibarua, Kariakoo ni mahali ambako ajira hiyo ilipatikana kwa wingi.



Sehemu ya Buguruni kwa Kimbegele sasa, kulikopatiwa jina kutokana na Mzee maarufu, KImbegele, aliyekuwapo zama zilizopita. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Hadi jina kuumbwa, ni mageuzi ya matamshi yanayopitia awamu mbalimbali. Hata hivyo kuna maana zingine zilizopo kwenye dhana, yakiwa hayana uhakika wa asilimia 100 kama ni kweli yalikuwa hivyo.

Kuna eneo la Mwanyamala, jijini Dar es Salaam ambalo maana yake kwa lugha ya Kizaramo ni 'mtoto nyamaza'. Wakati huo kulikuwa na pori kubwa, Kinamama wakikatiza eneo hilo, walikuwa wakiwambia watoto wao wasilie, ili wasisikike kwa maharamia.

Hata hivyo, kwa sasa mahali hapo hakuna pori tena. Ni mji maarufu wenye watu wengi, maarufu kama uswahilini.

### USHUHUDA WA KITAIFA

Wilayani Chunya Mkoa wa Mbeya, kuna kijiji kinachoitwa Godima, ambacho kilipewa jina hilo, kutokana na kifupi cha jina la Kiingereza 'Gold Mine', wakiwa na maana 'mgodi wa dhahabu'.

Mkoani Iringa penye barabara kuu ya lami wakati wa ujenzi wake, wapima ardhi wataalamu wa Kizungu walipokuwa kazini, walikuwa wanaelekezana wakitumia vipimo vya namna ya kutamkiana 'keep on zero' kwa alama ya kipimo iwe katika sifuri.

Ni bahati mbaya wenyeji hawakuweza kutamka kama wazungu, wakatamka kivyao, ikawa ndiyo jina la eneo hilo; 'keep on zero' ikawa 'kiponzero.'

Unapopataja Mpanda mkoani Katavi kuna sehemu inaitwa 'Milu'. Kumbe ni wenyeji walishindwa kutamka neno 'Mill' yaani usagishaji kwa sababu eneo hilo lilikuwa na kinu cha kusagia nafaka.

Morogoro, kupitia kilomita kadhaa nje ya mji katika barabara kuu ya kwenda Dar es Salaam, kuna sehemu inaitwa Kingolwira. Inasemekana, mtawala wa jadi wa Waluguru aitwaye Kingo, alikimbilia eneo hilo na kuweka makazi ya kudumu. Wenyewe Waluguru wakamtafsiri 'Kingo Kalowea'.

Jiji la Dodoma, linatokana na neno la asili 'idodomya' ambayo ni simulizi la embo kudidimia na kuzama kwenye tope. Wenyeji kila walipopita wakawa wanasema 'tembo amedidimia' kwa lugha yao, ndipo lilipopatikana jina hilo, huku Tanga maana yake ikiwa ni shamba.

'Kibo Alone' ni neno walilokuwa wakitamka wazungu kwenye sehemu ambayo walisimama na kuona kilele cha Kibo pekee bila kuona kilele cha Mawenzi.

Vyote ni eneo la Mlima Kilimanjaro. Wenyeji kwa kushinda kutamka hivyo, wakasema 'Kiborilonі', huku sehemu ya Kibosho ambayo ni kilele cha Kibo kilionekana vizuri zaidi, wazungu wakapaita 'KiboShow'. Wenyeji wao wakatamka Kibosho.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ROBERT MADINDA ALOYCE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2146.0083** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KAMPALA SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **KIL/SAM/RB/452319/2021.**

116557102

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**YASINI SHABANI SINTOO** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S2326/0552** iliyotolewa na MANGUANJUKI SEKONDARI mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **SIN/SIN/RB/525409/2021.**

116557002

## KUPOTEA KWA CHETI



**SUZANA FRANK MWAIKEKE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1770/0043** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia IMAGE SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/517958/2021.**

116556602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MARIAMU MWIDUCHI OMARI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 528 CVC** AINA YA TOYOTA CARINA. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KAH/ RB/528/2021.**

116556902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KIV COMPANY LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 154 ANM – TOYOTA LANDCRUISER.** Chassis namba **0003602.** Engine namba **0008590.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KIL/MOS/RB/480042/2021.**

116556502

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABUBAKARI HAMISI SARIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.3533/0122** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KAWE UKWAMANI SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. **9910830769766.**

116557402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER DEWAN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 155 DBL – TOYOTA RAV 4.** Chassis namba **ACA21008349.** Engine namba **1AZ0048671.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **ARU/ARU/RB/468707/2021.**

216557502

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-18

**Na Adam Fungamwango
(0716 350534)**

Kabla ya kupanda basi hilo, Tedi alimshauri Tom waipeleke simu ile kwenye ofisi za Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro ili Sam akamatwe kwa kosa la kutaka kuchapisha kuweka picha chafu za aliyekuwa mpenzi wake kwenye mtandao wa kijamii.

Tom alipinga. Hoja yake ni kwamba aachane na hilo kwa sababu hata wao hawakutumia njia halali ili kuipata simu ile.

"Kumbuka kuwa mimi ndiye niliyepanga mchezo mzima. Na wewe ukautekeleza kwa vitendo. Tukipeleka huko tatizo la polisi watashukuru sana, lakini watataka kujua simu ile ilipatikana vipi. Yaani ilichukuliwa vipi kutoka kwa mwenyewe. Hapo ndipo watakapogundua kuwa ulimuwekea vidonge kwenye pombe mmiliki wa simu. Hilo ni kosa. kazi ya kumkatama Sam ilibidi ifanywe na polisi wenyewe. Kwa hiyo wewe twende tu Dar." Tom akakumbuka kabla ya kufungua meseji ya Farida.

Macho ya Tom na Tedi sasa yakawa mbele kusoma meseji iliyoonekana kuwa ndefu, ambayo imetokwa kwa Farida. Mke wa Tom ambaye mpaka sasa alikuwa mkewe kisheria, kwani hakuwa na talaka.

"Kwako mume wangu Tom. Tulifunga ndoa, lakini hadi leo hii ni miezi mitatu sasa hujafaidi matunda ya kuwa na mke. Nilikutoroka wiki moja tu baada ya ndoa na kurejea Morogoro. Hukujua kuwa niko huku, lakini katika kunitafuta, ukagundua kuwa niko huku. Sijawahi kukupikia, kukufulia nguo na kukuonyesha chochote kile ambacho mke anapashwa kumfanyia mumewe. Hii yote ni kwa sababu ya hili ambacho umekichunguza na umekipata. Sababu kubwa ni Sam. Hata mimi pia inawezekana kuwa nilikuwa tatizo. Kosa langu mimi ni kutokukujulisha mapema. Nilitaka usijue chochote juu ya uhusiano wangu wa mwanzo na Sam. Lakini hiyo imenigharimu. Leo hii dunia nzima inajua kuwa nimekutoroka na nipo Morogoro. Tena nimerudi kwa mpenzi wangu wa zamani. Nililazimishwa, lakini ndiyo imeshakuwa. Nimejiona mimi ni mkosefu sana. Sina namna ya kufanya. Hata kama ukinikubali nikirejea kwako, lakini doa hili halitofutika kwako, kwa ndugu na jamaa zako wote. Hawatoniheshimu na hawatoniamini tena. Kwa yote yaliyotokea. Pamoja na kwamba nilikwambia unisamehe, lakini nimekaa na kutafakari, nimeona kuwa ni bora tu unipe talaka, utafute mwanamke mwingine. Mwanamke bora ambaye hana makandokando kama yangu. Nilichojifunza kwenye hili ni kwamba unapokuwa na mpenzi yoyote yule, jiepushe sana kurekodi au kupiga picha ambazo hazistahili. Siyo kama kama wapenzi wasipige picha, lakini kuna zile ambazo hazistahili kabisa kuonwa na watu wengine, kwani wakati mwingine wanaume huzifanya kama ni silaha kwao wanapotaka kuzitumia kwa manufaa yao. Hili ni somo kwa wanaume wenzangu wote."




**"Sijamfanya chochote kibaya. Sijafanya dhambi kubwa kwa mwenyezi Mungu ambayo haisameheki. Mungu nisaidie kama ni kweli hili linataka kutokea iwe kweli." Aliomba kimoyomoyo Tedi.**

Tom alimtazama Tedi. Tedi akamshangaa Tom. Wakatazama. Wakashangaana. Wakaendelea kusoma meseji hiyo ndefu.

"Kingine nilichojifunza kwenye hili na hata wanawake wenzangu pia wajifunze ni kwamba wanapoolewa ni lazima watakuwa walitoka kwenye mahusiano mengine. Hili ni jambo la kawada kumbe, wala si la kuficha. Mfanye mwanaume aliyekuoa aonekane shujaa. Mshindi kati ya wote ambao walikuwa na wewe. Walikutaka kimapenzi au kukuoa. Unapashwa umwambie mpenzi wake kama kuna tatizo na mpenzi wako wa zamani ili mume alitatue kwa ajili ya kulinda ndoa. Mimi ningekwambia mapema mume wangu kwamba Sam anataka kuvujisha picha zetu chafu kwa sababu tu ya kukubali kuolewa na wewe, ungeweza kuchukua hatua na akatiwa mbaroni kabla hajafanya hivyo. Lakini woga wangu ndiyo mauti yangu. Sikutaka umfahamu mwanaume wangu yoyote yule, wala uhusiano wowote wangu wa nyuma. Nimetafakari sana, nimekosa mume ambaye nilikupenda. Nakuacha nikiwa na uchungu. ningeweza kujinyonga, lakini nitakuwa namkosea Mungu. Ni dhambi kubwa. Nilichoona tu ni kwamba unipe talaka niangalie ustaarabu mwingine, lakini siwezi tena kurudi kwa Sam.

Wakati huo basi lilikuwa limeshafika Kibamba na wapenzi wao wawili waliteremka.

Wakakodisha taxi ya kuwapeleka nyumbani kwa Tom. Ni wakati ambao meseji nyingine ndefu iliingia.

Ilitoka kwa yule yule. "Mimi ni mtu mzima sasa. Nilivyoangalia niliona kabisa wewe na huyo dada aliyekuja hapa mna mahusiano. Sijui kama ni askari kweli au la. Nilivyomuona na yale maswali yake kama ni afande. Lakini kuna vitu nimeviona vinaniashiria kuwa ni wapenzi. Na mnapendana. Ni mwanamke mzuri, mrembo unaweza kumuoa. Mimi nimekwama. Haiwezekani tena. Dunia haitonielewa. Na wala wewe hutoeleweka. Ila tu naomba kama itawezekana muoe huyo dada." Ilimaliza meseji ya pili ambayo iliwashangaza kuliko ile ya kwanza.

Ni meseji ambayo ilimliza Tedi. Hata mwenyewe hakujua analia nini. meseji ya Farida imemliza, au ni machozi ya furaha baada ya kuonyeshewa taa ya kijani.

Ilibidi sasa Tom apate kibarua cha kumbembeleza. Wala hakutaka kumuuliza kinachomliza.

Msichana kutoka Singida, aliyepitia misukosuko kwenye maisha yake, akaenda Morogoro kusaka maisha. Akaangulia kuwa mhudumu wa baa akisumbuana na walevi wa kila aina na tabia za kila namna. Lengo ni kufanya kazi hiyo na kucheza upatu ili apate ada ya kujiunga na chuo cha urembo. Wakati anaanza kudunduliza anaangulia kwa mwanaume mmoja aliyetaka kupitisha naye usiku mmoja, lakini usiku unazaa siku na wiki kadhaa. Mbali na kazi aliyochukuliwa, anatumwa kazi moja ya hatari ya kumfuatilia mtu, kumelewesha na kumchukulia simu na nyaraka kadhaa. Anaifanikisha, akiwa anaifanya kwa ujira ya kulipiwa ada ya chuo cha urembo.

Hayo yote yamepita, lakini ghafla anaambiwa asirudi tena Singida, badala yake waongozane kwenda Dar es Salaam. Jiji ambalo hakuwahi kuliona, badala yake alikuwa anasimuliwa na baadhi ya wenzake aliokuwa akisoma nao wakienda kwa ndugu zao likizo.

Leo yupo Dar. Ni kama ndoto. Wakati akishangaa, inaonekana kabisa anaweza kuolewa na kuwa mama mwenye nyumba.

Tena na mwanaume ambaye ametokea kumpenda. Mwanaume ambaye tangu awe naye alijitofautisha na wengine ambao kazi yao, ilikuwa ni kumtumia tu kama ganda la mua na kumuacha akiteseka na ndoto zake za maisha ya baadaye, akiwa hajui maisha yake ya baadaye yatakuwaje.

Alichobakisha hapo Tedi ni kusikia kauli ya Tom tu. Ingawa alimwambia anataka awe mke wa pili, lakini aliona huo ulikuwa ni utani wa siku zote, kwani tangu akutane naye aligundua kuwa pamoja na ucheshi, alikuwa na utani.

"Sijamfanya chochote kibaya. Sijafanya dhambi kubwa kwa mwenyezi Mungu ambayo haisameheki. Mungu nisaidie kama ni kweli hili linataka kutokea iwe kweli." Aliomba kimoyomoyo Tedi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# HAKUNA TIMU DHAIFU MSIMU HUU -MAKOCHA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukamilika kwa raundi ya tano ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, baadhi ya makocha wameonyeshwa kufurahishwa na ushindani uliopo katika ligi hiyo mpaka sasa na kusema hakuna timu dhaifu msimu huu.

Kocha wa zamani wa Tanzania Prisons, Mohamed Rishard 'Adolf', aliliambia gazeti hili anafurahi kuona timu zote zinazoshiriki ligi hiyo msimu huu zimejiandaa kikamilifu na hata zile timu zinazoitwa au kujiita timu ndogo zinapambana kuanzia mwanzo wa msimu tofauti na miaka ya nyuma.

Adolf alisema miaka iliyopita timu ndogo zilionekana zikipambana zaidi katika muda wa lala salama kwa ajili ya kujinusuru kushuka daraja lakini sasa hali imekuwa tofauti.

"Ligi Kuu imekuwa nzuri na ina ushindani mkubwa, hata timu ndogo zimeanza kupambana tangu mwanzo na utaona kabisa mpaka sasa hakuna timu dhaifu," alisema Adolf, kiungo mkabaji wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars) na Pan African ya jijini Dar es Salaam.

Mbali na timu nyingi kuonekana kujipanga vyema, Adolf pia amesifia usajili uliofanywa msimu huu na timu zinazoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara kuwa ni mzuri, kiasi cha kutotofautiana viwango sana na wachezaji wenye majina makubwa.

"Tofauti yao ya viwango inakuwa nje ya uwanja tu na majina, lakini wakiingia uwanjani, unaona uwezo unafanana au hawatofautiani sana na wachezaji wenye majina makubwa," alisema kocha huyo.

Hata hivyo hakuacha kuwasifu makocha wanaofundisha timu hizo ambapo alisema hivi sasa wamekuwa wakija na mifumo mbalimbali, kutokana na timu wanazocheza nazo.

Naye Juma Mwambusi, alisema ligi ya msimu huu imeonyesha ushindani mkubwa mpaka sasa, kwani hata timu ndogo inapopoteza, basi ni kwa mbinde, huku timu kubwa zikipata ushindi kwa tabu.

Mwambusi alisema kila mechi sasa ni sawa na fainali na hakuna timu inayoondoka uwanjani na pointi tatu kirahisi.

Alisema pia timu zote zinaingia uwanjani zikiwa na nafasi sawa a hakuna ambaye anaingia kwenye mchezo akiwa na matokeo 'mfukoni'.

"Wachezaji wengi ni wazuri sana, timu hazitofautiani. Hata zilizopanda daraja msimu huu hazina tofauti na zilizopo kwenye Ligi Kuu kila mwaka. Ndiyo maana utaona hata ikifungwa mabao mawili inaweza kurudisha yote. Hii inapendeza sana na inaonyesha hakuna timu ndogo wala dhaifu." Alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga na Azam.

Ligi hiyo ya juu nchini kwa sasa imesimama kupisha kalenda ya mechi za kimataifa na itarejea tena kuanzia Novemba 19, mwaka huu.

## Kisiwani, Black Sailor dimbani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kisiwani FC inatarajiwa kuvaana na Black Sailor katika mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu ya PBZ Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Kisiwani, Khatib Omar Salum alisema tayari ameshafanya marekebisho ya makosa madogo yaliyokuwa katika kikosi chake na anaamini leo wataingia uwanjani wakiwa imara zaidi.

Kocha huyo alitaja moja ya changamoto aliyokuwa nayo ni baadhi ya wachezaji wa timu hiyo kutokuwa na uzoefu lakini ameshawaelekeza namna wanavyotakiwa kukabiliana na wapinzani.

"Wachezaji wangu wengi hawana uzoefu na Ligi Kuu Zanzibar, lakini pia wanakutana na ushindani hasa tunapocheza na timu za Unguja, tunaendelea kujipanga na kujiimarisha," alisema Khatib.

Aliongeza suala la mfumo wanaocheza si tatizo na anaamini wataendelea kupambana kwa sababu viwango vya wachezaji wa Zanzibar havitofautiani sana.

Naye Kocha Mkuu wa Black Sailor, Salehe Machupa alisema licha ya kuwakosa wachezaji wawili wa kikosi cha kwanza ambao ni majeruhi, bado anaimani ya kupata alama tatu katika mchezo huo wa leo.




Mshindi wa Jackpot bonus, Mjuane Mkumba wa jijini Dar es Salaam, akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni tano baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot ya SportPesa wiki hii ni Sh. milioni 642.6. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tanzanite, Uganda majaribuni CECAFA

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa Umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), inatarajia kukutana na wenyeji Uganda katika mechi ya kuwania Kombe la CECAFA itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa FTC Njeru ulioko katika Mji wa Jinja nchini humo.

Tanzanite Queens inahitaji ushindi wa aina yoyote ili kurejesha matumaini ya kushinda kombe la michuano hiyo itakayomalizika Jumanne.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na wamejiandaa kucheza kwa nidhamu zaidi.

Shime alisema mechi zote katika mashindano hayo ni ngumu na wao wataendelea kupambana mpaka katika mchezo wa mwisho.

"Akili zetu zote tunaiangalia Uganda, tunajua ni wenyeji na wenzetu wameshinda mechi zote, sisi pia tunahitaji ushindi dhidi yao, haitakuwa mechi nyepesi kwa kila upande," Shime alisema.

Mechi nyingine za mashindano hayo zitakazochezwa leo itakuwa ni kati ya Burundi dhidi ya Ethiopia wakati Eritrea watavaana na Djibouti.

Tanzanite Queens itamaliza mashindano hayo kwa kukutana na Djibouti wakati Burundi wataikabili Eritrea na Uganda itavaana na Ethiopia.

## Yondani, Makame vinara wa kadi

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA wa wachezaji watano, akiwamo kiungo mkabaji wa Namungo, Abdulaziz Makame na beki, Kelvin Yondani wa Polisi Tanzania, wanaongoza kwa kuonyeshwa na kadi nyingi za njano kwenye mechi za Ligi Kuu ambayo imefikia katika raundi ya tano.

Takwimu za ligi hiyo zinaonyesha Polisi Tanzania imekuwa kinara wa kuonyeshwa kadi nyingi za njano, ambapo wachezaji wake wanne wamelambwa kadi za njano, wakiwa na jumla ya kadi tisa mpaka sasa.

Makame, ambaye katika mechi ya dhidi ya Simba iliyochezwa Jumatano iliyopita, alilimwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya, Shomari Kapombe na Yondani kila mmoja ameonyeshwa kadi tatu za njano.

Wachezaji wengine ambao wameonyesha kadi tatu za njano kila mmoja ni Sospter Bajana wa Azam FC, Salum Salum kutoka Biashara United na Salmin Hoza anayeichezea Dodoma Jiji.

Nyota wengine wenye kadi mbili za njano ni Ismail Gambo, Abdallah Hamad na Kenny Mwambungu wa KMC, Benedict Mwamlagala na Mbarouk Hamza (Coastal Union), Nathaniel Chilambo (Ruvu Shooting), Pius Luchangula (Geita Gold), Abdallah Mfuko (Kagera Sugar) na Moses Kitandu (Prisons), Salum Chuku (Mbeya Kwanza), Ibrahim Mohamed,

## ZISIKUPITE

### MOURINHO ASAKA VIUNGO

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka kuwasajili viungo, Ruben Loftus-Cheek wa Chelsea na Harry Winks kutoka Tottenham ambao wote wana umri wa miaka 25. **(Corriere dello Sport)**

### ISAK AITAMANI EPL

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22, amesema "ana furaha kubwa" kucheza na Real Sociedad lakini "siku moja itakuwa vizuri akijiunga na Ligi Kuu England. **(Independent)**

### UNITED YAMKATAA RONALDO

MANCHESTER United haina mpango wa kumpa ofa ya kuwa kocha fowadi wao, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, baada ya ripoti kusema klabu hiyo inafikiria kufanya hivyo mara atakapostaafu. **(Star)**

### INTER YAMBANA CONTE

INTER Milan ipo tayari kumzuia kocha wao wa zamani na kocha mpya wa sasa wa Tottenham, Antonio Conte kusajili mchezaji yoyote kutoka kwao. **(Sky Italia, via Express)**

### NEWCASTLE SOKONI TENA

NEWCASTLE United inawania kumsajili kiungo wa Ufaransa, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 22 kutoka Marseille, ambako kwa sasa anacheza kwa mkopo akitokea Arsenal. **(Mirror via Foot Mercato)**

### ADAMU AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Southampton pamoja na Monaco ambazo zinashiriki Ligi Kuu Ujerumani, zinamwania nyota wa Red Bull Salzburg, Chukwubuike Adamu mwenye umri wa miaka 20 ambaye ni mzaliwa wa Nigeria lakini ana uraia wa Austria. **(Mail)**

### CARVALHO ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL inajiamini kuzipiku klabu kadhaa kwenye mbio za kuwania kumsajili, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 19 ambaye mkataba wake na Fulham unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja. **(Teamtalk)**

### TOMOYASU AITAJA SPURS

MLINZI wa Japan, Takehiro Tomiyasu mwenye umri wa miaka 22, amesema alikaribia kujiunga na Tottenham kabla ya kusajiliwa Arsenal kipindi cha majira ya joto. **(DAZN Japan, via Goal)**

### ATLETICO YAMTAKA BROCOVIC

KLABU ya Atletico Madrid inapanga kumpa ofa kiungo wa Croatia, Marcelo Brozovic mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho kule Inter Milan, huku akihusishwa na Manchester United na Newcastle. **(Fichajes)**

### CLARKE AGEUKA LULU

TIMU za Barnsley, Derby County, Millwall na Luton Town ni miongoni mwa klabu zinazomwania winga wa England mwenye umri wa miaka 20, Jack Clarke kutoka Tottenham wakati wa dirisha la Januari. **(Teamtalk)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# CONTE: UVUMILIVU UNAHITAJIKA SPURS

●●●Afunguka kikosi chake kilivyojiweka kwenye mazingira magumu katika...

**LONDON, England**

ANTONIO Conte amesema uvumilivu unahitajika baada ya kuiongoza Tottenham Hotspur katika "mchezo wa vurugu" dhidi ya Vitesse kwenye Ligi ya Europa Conference.

Spurs walipata ushindi wa mabao 3-2 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur juzi, lakini walijitengenezea wenyewe mambo magumu baada ya kuongoza kwa mabao matatu ya Son Heung-min, Lucas Moura na la kujifunga la Jacob Rasmussen ndani ya nusu ya kwanza.

Bao la ufunguzi la Son limemaanisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini amefunga bao la kwanza kwa Spurs katika kila mechi ya kwanza ya kocha mpya kati ya watatu katika siku za hivi karibuni.

Rasmussen alisawazisha makosa yake kwa kufunga bao kabla ya Matus Bero kufunga la pili, na kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwa Cristian Romero kukawaweka wenyeji kwenye presha kubwa.

Vitesse hawakusawazisha, lakini wakawapoteza kwa kadi nyekundu, Danilho Doekhi na golikipa, Markus Schubert.

Conte alichagua kikosi imara kwenye mchezo huo, akifanya badiliko moja tu katika kikosi alichokiteua Nuno Espirito Santo aliyefukuzwa, dhidi ya Manchester United wikendi iliyopita akiwaanzisha Son na Harry Kane kwa mara ya kwanza kwenye michuano hiyo.

Lakini wakati Spurs ikirudi kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Everton Jumapili kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa, Conte ameonya itamchukua muda kutengeneza timu anayoitaka.

"Ulikuwa mchezo wa aina yake. Kwa kawaida sipendi mchezo wa aina hii, mchezo wa vurugu unamaanisha chochote kinaweza kutokea.

"Na wakati huo huo, nilifikiri tulitakiwa kushinda na tulishinda," alisema Conte akiiambia BT Sport.

"Tulitakiwa kushinda 3-0 halafu tukaruhusu mabao mawili ambayo tulitakiwa kuyaepuka. Baada ya kadi nyekundu tulikuwa kwenye wakati mgumu. Kushinda huku upo kwenye wakati mgumu ni nzuri kwa timu na wachezaji."

**HABARI MICHEZO**

MECHI KALI
HOME
MANCHESTER UTD
4.22 | 3.93 |1.76
MANCHESTER CITY
AWAY
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 642



# DESCHAMPS AMTEMA GIROUD UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**

DIDIER Deschamps amewaambia wachezaji wa Ufaransa kumaliza kazi waliyoianza kwa kuhakikisha wanafuzu michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, huku akimtema Olivier Giroud kwenye kikosi chake.

Baada ya kuwa kwenye wakati mbaya katika michuano ya Euro 2020, ambapo Ufaransa ilikuwa ikipewa nafasi kubwa, ilitolewa na Uswisi hatua ya 16, na baadae Oktoba wakashinda taji la Ligi ya mataifa ya Uefa.

Na sasa wanarudi tena kwenye michuano ya kimataifa katika mechi za kufuzu kombe la Dunia ambapo watacheza nyumbani na Kazakhstan Novemba 13 na wataifuata Finland siku tatu baadae.

Kama wakiifunga Kazakhstan, watakuwa wamejihakikishia nafasi ya kufuzu muchuano ya kombe la Dunia mwakani.

Na Deschamps anataka hilo lifanyike kwenye mchezo wa kwanza kwa kadili inavyowezekana, akisema: "Unajua nini kilichotokea kipindi cha majira ya joto, kwa kuondolewa kwetu mapema kwenye michuano ya Euro.

"Hili halijatuzuia sisi kuendelea kufanya vitu vizuri huku tukiwa na furaha ya kushinda taji la Ligi ya mataifa ya Uefa."

Hakukuwa na mshangao mkubwa kwa kikosi cha wachezaji 23 wa Deschamps, ambacho kilitajwa juzi huku straika mkongwe, Giroud akiachwa.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye anashika nafasi ya pili wa wafungaji wa muda wote wa Ufaransa, kwa mara ya mwishi aliicheza dhidi ya Uswisi kwenye Euro pale mjini Bucharest, Juni.

# Zaha aomba kuachwa Ivory Coast



**MANCHESTER, England**

WILFRIED Zaha hana mpango wa kustaafu kuichezea timu ya taifa ya Ivory Coast licha ya kuomba kutokuitwa kwenye timu hiyo.

Kocha wa timu ya Ivory Coast, Patrice Beaumelle, alisema anajua kuwa ametengeneza sintofahamu na kutafsiliwa vibaya kutokana kumuacha Zaha kwenye kikosi hicho.

Lakini Beaumelle amebainisha kwamba, alizungumza na Zaha na walikubaliana kuwa amwache kwenye michezo ya kufuzu kombe la Dunia inayofuata dhidi ya Msumbiji na Cameroon.

"Nilikutana na Zaha na tulikubaliana kwamba, anaomba asicheze dhidi ya Msumbji na Cameroon," alisema Beaumelle.

Uamuzi uliofanyika kutokana na nafasi waliyonayo kwenye kundi na pia matatizo ya majeruhi ya mara kawa mara ya Zaha anapokwenda kuichezea timu yake ya Ivory Coast.

Mara ya mwisho kuitumikia timu yake ya taifa na kupata majeruhi ilisababisha Zaha kukosa kuichezea Crystal Palace dhidi ya Arsena.

Kukosekana kwa Zaha kwenye michezo ya kimataifa ni sherehe kwa timu yake ya Crystal Palace sababu watakuwa na uhakika wa kuwa hatoweza tena kukosa mchezo wa ligi kuu baada ya kupisha mapumziko ya michezo ya kimatifa.

2,668,240

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/11/21 | 18:00 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 2.42 | 3.14 | 3.04 |
| 02. 06/11/21 | 18:00 | Blackburn vs Sheffield Utd | 2.32 | 3.29 | 2.89 |
| 03. 06/11/21 | 18:00 | Luton Town vs Stoke City | 2.27 | 3.21 | 3.06 |
| 04. 06/11/21 | 18:00 | Barnsley vs Hull City | 2.44 | 3.09 | 2.89 |
| 05. 06/11/21 | 20:30 | Alaves vs Levante | 2.55 | 3.05 | 2.95 |
| 06. 06/11/21 | 20:30 | Blackpool vs QPR | 2.44 | 3.28 | 2.74 |
| 07. 07/11/21 | 17:00 | Everton vs Tottenham | 2.65 | 3.15 | 2.75 |
| 08. 07/11/21 | 17:00 | Nantes vs Strasbourg | 2.38 | 3.23 | 2.98 |
| 09. 07/11/21 | 17:00 | Leeds vs Leicester | 2.85 | 3.45 | 2.39 |
| 10. 07/11/21 | 17:00 | Udinese vs Sassuolo | 2.47 | 3.44 | 2.75 |
| 11. 07/11/21 | 20:30 | Osasuna vs Real Sociedad | 2.94 | 3.24 | 2.43 |
| 12. 07/11/21 | 22:45 | Rennes vs Lyon | 2.89 | 3.48 | 2.32 |
| 13. 07/11/21 | 23:00 | Betis vs Sevilla FC | 2.80 | 3.21 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE

"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 06 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4041 | Sivasspor vs Giresunspor | 1.88 | 3.46 | 3.95 |
| 14:00 | 1368 | Arsenal Tula vs Ufa | 2.45 | 3.10 | 2.86 |
| 14:00 | 3927 | CD Trofense vs Rio Ave | 3.52 | 3.27 | 2.02 |
| 15:30 | 2667 | Manchester Utd vs Manchester City | 4.22 | 3.93 | 1.76 |
| 16:00 | 4374 | Espanyol vs Granada | 1.87 | 3.36 | 4.41 |
| 16:00 | 4529 | Antalyaspor vs Altay | 2.51 | 3.25 | 2.71 |
| 16:00 | 4860 | Yeni Malatyaspor vs Basaksehir | 3.16 | 3.36 | 2.17 |
| 16:30 | 2706 | Dinamo Moscow vs FC Krasnodar | 2.80 | 3.29 | 2.39 |
| 16:30 | 3615 | Kryliya Sovetov vs FK Khimki | 1.86 | 3.39 | 4.02 |
| 16:30 | 5077 | Kaizer Chiefs vs Orlando Pirates | 2.78 | 2.93 | 2.64 |
| 16:30 | 5838 | FC Liefering vs Blau Weiss Linz | 2.11 | 3.51 | 2.93 |
| 17:00 | 5456 | Spezia vs Torino | 3.39 | 3.49 | 2.09 |
| 17:30 | 3368 | VfL Bochum vs Hoffenheim | 3.64 | 3.78 | 1.90 |
| 17:30 | 3533 | Bayern Munchen vs SC Freiburg | 1.17 | 7.81 | 12.01 |
| 17:30 | 4879 | Stuttgart vs Arminia Bielefeld | 1.85 | 3.69 | 3.94 |
| 18:00 | 1077 | Brentford vs Norwich City | 1.62 | 3.86 | 5.41 |
| 18:00 | 1162 | Stellenbosch vs Golden Arrows | 2.15 | 3.14 | 3.38 |
| 18:00 | 1183 | Cliftonville Belfast vs Dungannon Swifts | 1.26 | 5.39 | 8.27 |
| 18:00 | 1506 | St Johnstone vs St Mirren | 2.29 | 3.06 | 3.21 |
| 18:00 | 1595 | Peterborough vs Fulham | 5.89 | 4.32 | 1.47 |
| 18:00 | 1668 | Barnsley vs Hull City | 2.24 | 3.14 | 3.19 |
| 18:00 | 1690 | Ayr United vs Inverness | 3.17 | 3.02 | 2.28 |
| 18:00 | 1810 | Hamilton vs Arbroath | 2.74 | 3.38 | 2.36 |
| 18:00 | 2059 | Nottingham vs Preston | 2.15 | 3.19 | 3.33 |
| 18:00 | 2120 | Hearts vs Dundee Utd | 1.72 | 3.49 | 4.82 |
| 18:00 | 2170 | West Bromwich vs Middlesbrough | 1.76 | 3.57 | 4.31 |
| 18:00 | 2938 | Kilmarnock vs Partick Thisle | 2.07 | 3.32 | 3.32 |
| 18:00 | 3028 | Crystal Palace vs Wolverhampton | 2.47 | 3.11 | 3.01 |
| 18:00 | 3114 | Dunfermline vs Morton | 2.05 | 3.23 | 3.48 |
| 18:00 | 3317 | Cardiff vs Huddersfield | 2.31 | 3.19 | 3.00 |
| 18:00 | 3595 | Aberdeen vs Motherwell | 1.76 | 3.45 | 4.64 |
| 18:00 | 4204 | Millwall vs Derby | 1.82 | 3.29 | 4.42 |
| 18:00 | 4853 | Bournemouth vs Swansea | 1.72 | 3.54 | 4.62 |
| 18:00 | 4930 | Queen of South vs Raith Rovers | 3.33 | 3.33 | 2.07 |
| 18:00 | 5234 | Luton Town vs Stoke City | 2.34 | 3.19 | 2.95 |
| 18:00 | 5447 | Blackburn vs Sheffield Utd | 2.75 | 3.34 | 2.40 |
| 18:00 | 5778 | Birmingham vs Reading | 1.82 | 3.48 | 4.11 |
| 18:00 | 5867 | Coventry vs Bristol City | 1.74 | 3.59 | 4.42 |
| 18:15 | 1503 | Celta Vigo vs Barcelona | 3.21 | 3.41 | 2.20 |
| 18:30 | 1833 | FC Vizela vs GD Estoril | 2.47 | 3.11 | 2.87 |
| 19:00 | 4334 | Besiktas vs Trabzonspor | 2.36 | 3.39 | 2.80 |
| 19:00 | 4793 | Austria Vienna vs RB Salzburg | 6.56 | 4.82 | 1.35 |
| 19:00 | 5870 | Sochi vs CSKA Moscow | 2.31 | 3.19 | 2.99 |
| 20:00 | 3824 | Juventus vs Fiorentina | 1.69 | 3.90 | 4.74 |
| 20:30 | 2007 | Alaves vs Levante | 2.49 | 3.04 | 3.04 |
| 20:30 | 3366 | RB Leipzig vs Borussia Dortmund | 1.99 | 3.83 | 3.33 |
| 20:30 | 5865 | Blackpool vs QPR | 2.78 | 3.32 | 2.38 |
| 22:00 | 3252 | Willem II Tilburg vs Sparta Rotterdam | 2.13 | 3.48 | 3.09 |
| 22:45 | 2436 | Cagliari vs Atalanta | 5.40 | 4.60 | 1.52 |
| 23:00 | 1818 | Real Madrid vs Rayo Vallecano | 1.42 | 4.81 | 6.84 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# DEMBELE 'PANCHA' TENA BARCELONA



**BARCELONA, Ufaransa**

BARCELONA imetangaza, Ousmane Dembele amepata maumivu ya misuli, ikiwa ni siku mbili tu kwa Mfaransa huyo akiwa amerudi kuichezea timu hiyo baada ya kutoka kufanyiwa upasuaji wa goti uliomweka nje ya dimba kwa miezi mitano.

Dembele alicheza mchezo wake wa kwanza msimu huu wakati alipoingia dakika ya 65 kuchukua nafasi ya Gavi huku Barca ikishinda bao 1-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Dynamo Kiev, Jumanne iliyopita.

Hata hivyo, klabu hiyo ilitangaza juzi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 "ameumia nyama za misuli."

Fowadi huyo wa zamani wa Borussia Dortmund amekuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara tangu uhamisho wake wa fedha kubwa kutua hapo Katalunya mwaka 2017.

Klabu hiyo pia ilithibitisha, Sergino Dest atakosa mchezo wa mwishoni mwa wiki dhidi ya Celta Vigo.

Haijulikani kama atakuwa fiti baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Kwa sasa Barca wapo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na imeshinda mechi moja tu kati ya tano zilizopita, ikipoteza tatu.

# Sancho atemwa kikosi cha England

**LONDON, England**

JADON Sancho ameachwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya England na kocha, Gareth Southgate.



Kuachwa kwa winga huyo kunatokana na kuwa na kiwango kisichovutia na kukosa nafasi ya kucheza mechi nyingi tangu aliposajiliwa kipindi cha majira ya joto pale Manchester United.

Kieran Trippier na Jesse Lingard pia wameachwa kwenye kikosi cha wachezaji 25 kwa ajili ya mechi dhidi ya Albania na San Marino.

Southgate alisema: "Kwa Jesse na Jadon hawachezi mara nyingi ikilinganishwa na wachezaji wengine kwenye nafasi zao.

"Najua watu wanasema kwamba, nawaacha mara kwa mara, lakini sidhani kama hilo lina maana.

"Kama unacheza mara kwa mara katika klabu yako, unakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kupata nafasi kwenye timu ya taifa."

Jude Bellingham amerudi kwenye kikosi baada ya kupumzishwa Oktoba, huku Ben Chilwell naye akiitwa baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kule Chelsea pamoja na nahodha wa Southampton, James Ward-Prowse.

# Michezo

Jumamosi Novemba 6 , 2021

Nipashe




## Conte: Uvumilivu unahitajika Spurs

UKURASA 21



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (katikati), akizungumza na wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inajiandaa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Madagascar. Kulia ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa na kushoto ni nahodha wa Stars, John Bocco. Katika kikao hicho, Sh. bilioni 1.6 zilikusanywa kusaidia maandalizi ya timu hiyo. **PICHA: TFF**

# NABI - MOTO WA YANGA HAUZIMIKI

## ●●●Lengo ni kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi na…

**Na Saada Akida**

ILI kuhakikisha kikosi chake kinaendelea kuwa kwenye ubora na kiwango kizuri, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema ataendelea kuwaimarisha wachezaji wake kwa sababu wanahitaji kupata pointi tatu katika kila mechi watakayocheza kwenye Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kupata ushindi katika mechi zote tano walizocheza, ikiwa ndio timu pekee iliyoshinda michezo yote mpaka sasa.

Nabi alisema matokeo ni mazuri ingawa amekiri haikuwa kazi rahisi kwa nyota wake kuvuna pointi 15 ambazo zimewaweka katika kilele cha msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

"Nina furaha, unapocheza mechi tano na zote ukapata ushindi, wote tunajua ligi ni ngumu, ina ushindani, timu zote zimejipanga kusaka pointi, kwa sababu hiyo hatutazubaa, tunahitaji kuona tunazidi kuimarika," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza ligi bado iko katika hatua za mwanzo, hivyo wanahitaji kuendelea kufanya vizuri kwa ajili ya kutimiza malengo yao kama ambavyo timu nyingine zilivyojipanga.

"Kila timu imejipanga, tumeanza msimu vizuri, tunahitaji kuendelea hivi hivi, tunakutana na changamoto ya kucheza kwenye viwanja tofauti, lakini hili tunakutana nalo wote, huwezi kulizungumzia, kikubwa ni kuendelea kupambana ili kupata kile tunachokitarajia," Nabi alisema.

Aliongeza ushindani wa namba kwenye kikosi chake unasaidia kuimarisha ubora wa timu na licha ya kupata ushindi kwenye mechi walizocheza, bado hakuna mchezaji mwenye uhakika wa namba kwenye kikosi cha kwanza.

"Kila mchezaji ana ubora wake, kupata nafasi ya kucheza au kutopata ni suala la wakati, kikosi kitakachoanza kinatokana na mfumo na aina ya mpinzani tunayekutana naye, kuna mchezaji mwingine anakuwa bora anapokutana na timu A, lakini huyo huyo anakaa nje unapocheza na timu B," Nabi aliongeza.

Naye Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh alisema kikosi chao kinatarajia kurejea mazoezini leo kwa ajili ya kujiandaa kuwafuata Namungo FC baada ya kumaliza mapumziko ya siku mbili.

"Tutaendelea na mazoezi kwa wale wachezaji ambao hawajaitwa katika timu za Taifa, tunahitaji kuwa na mwendelezo ule ule mara ligi itakaporejea, kila mchezaji anatakiwa kuwa tayari kupambana kwa ajili ya timu," alisema meneja huyo.

Namungo FC itaikaribisha Yanga katika mchezo wa raundi ya sita utakaochezwa Novemba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

Yanga inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ikiwa na pointi 15, ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 11, Polisi Tanzania na Dodoma Jijin FC wanafuatia wakiwa na pointi 10 kila moja huku Kagera Sugar yenye pointi nane ikikamilisha 'Tano Bora'.

## Mrithi wa Gomes kujulikana J'tatu

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA bado na machungu ya kutolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba inatarajiwa kumtangaza kocha wake mpya atakayechukua mikoba iliyoachwa na Mfaransa Didier Gomes ifikapo Jumatatu, imefahamika.

Gomes aliamua kujiuzulu nafasi yake mwezi uliopita baada ya timu hiyo kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez aliliambia gazeti hili mchakato wa kusaka kocha mpya umekamilika na wakati wowote kuanzia Jumatatu atawekwa hadharani.

Barbara alisema walipokea maombi kutoka kwa makocha 94, saba kati ya hao ni kutoka Afrika, akiwamo raia wa Senegal, Lamine N'Diaye, ambaye ni kocha wa zamani wa klabu ya Horoya ya Guinea.

"Tunataka kocha ambaye amekidhi vigezo vyote vinavyotakiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), uzoefu wa soka la Afrika na mafanikio," alisema Ofisa Mtendaji huyo.

Mbali na mechi za Ligi Kuu, Simba pia inajiandaa na mechi ya mchujo ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambapo itaanza kwa kuwakaribisha Red Arrows ya Zambia Novemba 28, mwaka huu na kurudiana Desemba 5, mwaka huu huko Zambia.

Naye Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ally Shatry, alisema jopo maalum linalosimamia mchakato huo wa kutafuta kocha limeshakamilisha mchakato wa awali na sasa wanaelekea ukingoni kukamilisha mchakato huo.

"Huu mchakato ukiangalia kwa jicho la kawaida utaona ni mwepesi, kutokana na maombi yaliyokuja kuna kazi kubwa na tunataka kocha mwenye ufundi mwingi, kucheza soka la chini, atakayeifanya Simba iwe na uwezo zaidi, kutupa mafanikio ndani na nje katika mashindano yote na kuleta ushindani," alisema Shatry.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >